SportPesa
TZS. 1,013,643,920
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Waiba** jeneza msikitini kisha kutoweka nalo

UKURASA 3



**CHRISTENSEN AKUBALI MIAKA MITANO BARCELONA**

UKURASA 22

Nipashe
Jumatano Machi 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580879
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# TUJIANDAE

## Watu 33,726 wapata corona na wengine 800 wafariki dunia

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Abeida Rashid Abdalla, baada ya kuwasili katika Viwanja vya Maisara Zanzibar jana, kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: IKULU**

• **Rais** Samia ahadharisha hali ngumu kiuchumi, kutokana na vita Ukraine...*Ukurasa 2*


## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**SHAHIDI ALIKANA GENGE UHALIFU KESI SABAYA**

SHAHIDI wa nne wa utetezi, John Odemba, katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa...

**UKURASA WA 8**

**TANZANIA MWENYEJI MKUTANO WA UTALII**

TANZANIA imetia rasmi saini mkataba wa kukubali kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa utalii wa...


Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwa amezongwa na wanachama wa chama hicho, baada ya kuwasili kwenye kongamano la Siku ya Wanawake Duniani, lililoandaliwa na Baraza Kuu la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) Taifa, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



## Mbowe asema hakutarajia kuitwa Ikulu kuteta na Rais

• **Asisitiza** wanawake ni muhimu ndiyo maana amekubali wito licha ya uchovu...
*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** PABLO APATA JEURI YA SILAHA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, wakijiandaa kukata keki kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, katika chumba cha habari cha TGL, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. **Picha zaidi Uk. 19 PICHA: JOHN**

## VITA VYA UKRAINE

# Rais Samia asema vitatuumiza kiuchumi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine, vitasababisha hali ngumu kimaisha ikiwamo kupanda kwa bei ya mafuta na mfumuko wa bei.

Kutokana na hali hiyo, Rais amewataka Watanzania kujiandaa kukabiliana na magumu ya kiuchumi yatakayojitokeza, kwa kuwa hali halisi imeonyesha dalili za yajayo.

Mkuu wa Nchi alitoa kauli hiyo jana alipohutubia kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliofanyika katika Viwanja vya Maisara mjini Unguja.

"Tanzania hatutanusurika na migogoro ya vita vya Urusi na Ukraine ambapo zipo dalili za kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu za vyakula," alifafanua katika hadhira hiyo iliyohudhuriwa pia na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema Tanzania haitanusurika dhidi ya mgogoro huo kati ya mataifa hayo makubwa, akibainisha kuwa tayari dalili zimeanza kujitokeza, ikiwamo kupanda kwa bei ya vyakula na mafuta duniani.

Rais Samia, hata hivyo, alidokeza kwamba serikali imejipanga kukabiliana na hali hiyo huku akiwataka wananchi wasikate tamaa na mapito hayo, dhidi ya hatua zinazoendelea za kuijenga nchi.

"Tufunge mikanda kwa kushikamana na hatimaye tutayashinda mambo yote hayo yanayotukabili kama tulivyoshinda vita vya UVIKO- 19," aliwahimiza Watanzania katika tukio hilo ambalo mantiki ya dhima yake iliwaangalia wanawake kuinuka kiuchumi na kuufikia usawa wa kijinsia nchini.

Alikumbusha mapito ya awali, wakati huo akiwa Makamu wa Rais, kwamba taifa lilikumbwa na janga la ugonjwa wa UVIKO-19, lakini mbinu ya kujihami huku umma haujajifungia ndani tofauti na nchi majirani, ilileta matokeo chanya na kuyavuka mapito.

Kuhusu mikakati ya kuleta usawa wa kijinsia nchini, Rais alisema serikali yake imejipanga kuwawezesha wanawake kwa kuwapatia mitaji katika kila mkoa nchini.

Alisema serikali tayari imekamilisha mazungumzo na makubaliano na benki za CRDB na NMB ambazo zimefungua madirisha ya mikopo yenye masharti nafuu nchini kote.

"Tumejipanga kuwawezesha wanawake kiuchumi, katika mikoa yote tutaweka madirisha na mitaji ya fedha ikiwa na masharti nafuu ya mikopo. Tayari benki za CRDB na NMB tumezipa kazi za kusimamia masuala hayo," alisema.

Rais Samia pia aliwataka wanawake kusimama kidete kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa kuwa waathirika wakubwa ni wanawake na watoto.

Pia aliwataka wananchi kuacha muhali na kuwa tayari kutoa taarifa za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia mbele ya vyombo vya sheria kwa hatua za kisheria.

"Huu ni wakati wa kuachana na mila potofu na kuacha muhali kwa kutoa taarifa za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia ili kuona kwamba tunavikomesha moja kwa moja," aliagiza.

Akizungumzia uhifadhi wa mazingira, Rais Samia aliitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulinda mazingira na kuacha kuharibu miamba inayovilinda visiwa vya Unguja na Pemba.

Rais alisema visiwa vya Zanzibar vinakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, akisisitiza kuwa juhudi za makusudi zinahitajika kuchukuliwa kudhibiti kasi ya maji ya bahari na matumbawe.

"Mheshimiwa Rais (Dk. Mwinyi) tusimamishe mara moja ukataji wa miamba ya matofali kwa ajili ya kukata matofali. Miamba ile ndiyo iliyozuia visiwa vya Unguja na Pemba, ni hatari kuikata," alionya.

Rais Samia pia aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika sensa ya watu na makazi ambayo lengo lake kubwa ni kujua idadi ya wananchi nchini na shughuli zao za maendeleo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema ataendelea kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuwaunga mkono wanawake ili wapige hatua kubwa kiuchumi na maendeleo, akiahidi kuwapa nafasi zaidi za uongozi na kisiasa.

"Nassor Ahmed Mazrui ataendelea kuwa Waziri wa Afya pekee na kwa sasa namtafuta pacha wa Waziri Dk. Dorothy Gwajima, ambaye atahusika na masuala ya jinsia," alisema Dk. Mwinyi.

# Mbowe asema hakutarajia kuitwa Ikulu kuteta na Rais

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amefunguka kilichompeleka Ikulu kuteta na Rais muda mfupi baada ya kutoka gerezani.

Mbowe aliiambia hadhira ya kinamama wa chama chake jana mjini hapa kuwa, aliamua kuitumia fursa hiyo adimu aliyoisaka kwa bidii, ikiwamo kuandika barua kadhaa za maombi hata kabla ya kwenda mahabusu gerezani, lakini hakufanikiwa.

"Natambua kumekuwapo na mijadala mbalimbali pamoja na taharuki ya jinsi nilivyoweza kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan Ikulu ambapo taharuki hii nitaijibu hapa leo (jana). Kwa muda wote gerezani nilitumia muda wangu kusali na kumwomba Mungu," alisema.

Mbowe alidokeza kwa ufupi maudhui ya kikao chao yaliegemea kwenye maridhiano ya kisiasa akiyapata tathmini kwa kauli 'yalikuwa mazuri' pia akitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais kwa uamuzi wake huo.

Alisema kuwa kabla ya kwenda gerezani, alimwandikia barua Rais Samia kuomba kukutana naye, lakini hakupata nafasi hiyo huku akikumbusha kwamba hata kabla aliomba mara tatu kukutana na mtangulizi wa Rais Samia, Hayati Dk. John Magufuli, hakujibiwa.

Mbowe alisema alipata kukutana mara kadhaa na Rais Magufuli kwenye misiba na matukio mengine, lakini hakupata fursa ya kumweleza wazi.

"Ndugu zangu Watanzania; kesi yangu ilipofutwa nilipokea ujumbe kutoka Kwa Rais Samia, alitaka nikutane naye haraka iwezekanavyo. Ninakumbuka Rais pekee ambaye wapinzani tulipata kukutana naye ni Jakaya Kikwete.

"Nilipopata mwaliko nilipotoka gerezani, niliahidi nitafika. Niliondoa uchungu niliokaa gerezani. Nichukue nafasi hii kumshukuru Rais Samia kwa kunipa nafasi ile pamoja na mazungumzo mazuri yalivyokwenda. Nampa ahsante kwa kufungua malango ya maridhiano," alisifu.

Mbowe alisema kuwa Rais Samia amekuwa Rais wa kwanza kuzungumza naye kwa nia ya kutaka kutafuta mwafaka wa kisiasa, kuondoa maumivu ya kisiasa na kuweka misingi bora ya demokrasia nchini.

"Ndugu zangu; kama mnavyotambua kwa zaidi ya siku 200 nilikuwa nimetiwa nguvuni na vyombo vya dola pamoja na waliokuwa walinzi wangu: Khalipan; Adam Kasekwa; na Mohamed Ling'wenya ambao nipo nao hapa. Makamanda hawa wamekaa gerezani siku 577 ama wiki 82, lakini wote kwa pamoja ninazungumza kwa niaba yao wanawashukuru sana," alisema.

Mbowe alisema kuwa mawakili walifanya kazi kubwa wakiongozwa na Wakili Peter Kibatala, pia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari vilifanya kazi kubwa kuupa taarifa umma na kuifanya kesi hiyo kufuatiliwa zaidi.

"Kuwa kupitia vyombo vya habari ulimwengu uliweza kubaini kuwa Mbowe ni gaidi kweli ama Mbowe si gaidi," alisema na kutoa pongezi kwa mabalozi wa nchi mbalimbali walioamua kufuatilia kesi hiyo usiku na mchana na kuakisi alichokiita nguvu ya familia ya CHADEMA.

"Nililetewa mchele na kila aina ya msaada nikiwa gerezani pamoja na fedha za kusaidia watoto wetu na familia zetu. Hakika nasema Mungu awabariki sana na sina cha kuwalipa zaidi ya mimi kusimama kutetea kila Mtanzania," alisema.

Mbowe pia alizipongeza mamlaka zote zilizofanya uamuzi wa kutoendelea na kesi hiyo, akisifu kuwa uamuzi wao umerejesha furaha kwa familia ya CHADEMA.

"Maandiko yanafundisha kushukuru kwa kila jambo. Siku zote nimekuwa nikihubiri kuwa CHADEMA kamwe hakitakuwa chama cha kisasi," Mbowe alisisitiza na kudai kufanyika kile alichokiita ukatili mkubwa dhidi ya chama chao kwenye uchaguzi lakini kamwe hawatahubiri sera za chuki.

Alisema CHADEMA ni chama cha kidemokrasia na hakijapata kuwa chama kibaraka kwa chama tawala na hakitafanya hivyo, akisisitiza kuwa wajibu na misingi ya chama chake imejengwa kujitegemea na kamwe hakitakuwa tayari kubebwa na watu.

"Tulikataa na hakika hatutakubali kuwa watumwa wa fedha za watu na wale wenye tamaa ya fedha hatutasita kuwaomba waende zao," Mbowe alionya.

Alisisitiza kuwa CHADEMA haikuundwa ili viongozi wa sasa wapate faida, bali kipo kwa ajili ya vizazi vijavyo kufurahia matunda ya chama hicho na katika ujenzi wa chama, hakuna aliye bora kuliko mwingine.

Alidai kumekuwapo nguvu kubwa za kutaka chama hicho kife, akionya kuwa "watambue kuwa nguvu wanazotumia kuua chama zinasaidia kukijenga zaidi chama kuliko kubomoa".

"Ndugu zangu Watanzania; mtakumbuka tarehe 21 Aprili nilizungumza nanyi. Ndani ya hotuba hiyo nilichambua kwa kina... miezi mitatu nilitiwa nguvuni," Mbowe alisema na kusisitiza hataacha kukemea vitendo vya utekaji na kufungana ovyo.

**USAWA WA KIJINSIA**

Katika mkutano huo uliokuwa mahususi kwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Mbowe alisema anatambua uzito wa mwanamke na ndiyo maana ameamua kutopumzika na badala yake kuhudhuria maadhimisho hayo.

Alisema wanawake wamekuwa na nguvu ndani ya CHADEMA na kwake kama mwasisi wa chama, anatambua walipoanza miaka 30 iliyopita, ilikuwa vigumu kukusanya wanawake watano kwa wakati huo.

Mbowe alisema Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) sasa lina nguvu kubwa kuliko mabaraza ya vyama vingine vya siasa nchini licha ya vikwazo kadhaa walivyopitia kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita.

Alisema chama hicho kitaendelea kuwaheshimisha wanawake kutokana na nguvu kubwa na misingi bora waliyonayo ya kukitumikia chama hicho na taifa kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# 33,726 wapata corona, 800 wafariki dunia

Na Maulid Mmbaga

WATU 33,726 wamethibitika kuwa na ugonjwa wa UVIKO-19, huku 800 wakipoteza maisha kwa kipindi cha Machi, mwaka juzi hadi Machi 4, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, ilisema idadi hiyo ni kati ya 471,965 sawa na asilimia 7.1 na waliopoteza maisha ni asilimia 2.5.

Alisema kuanzia Februari 5 hadi Machi 4, mwaka huu, kulikuwa na wagonjwa walioripotiwa kupata ugonjwa huo kati ya watu 31,090 waliopimwa na vifo vinane na idadi kwa kila mkoa kwenye mabano ni Mwanza (watano), Dodoma (wawili) na Kagera mmoja.

Pia alisema katika wagonjwa hao visa 290 vilivyothibitika, mkoa wa Dar es Salaam umeongoza kwa kuwa na wagonjwa 175.

Dk. Sichwale pia alibainisha kuwa katika kipindi hicho, wagonjwa wapya 136 walilazwa, kati yao 128 sawa na asilimia 94.1 hawakuchanja na mahututi walikuwa wanne.

"Serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo kote nchini ili kuwawezesha wananchi kupata kinga. Mpaka kufikia Machi 4, mwaka huu, zaidi ya dozi milioni 9.8 za chanjo ya UVIKO-19 zilipokewa nchini," alibainisha Dk. Sichwale.

Aliongeza kuwa toka suala la uchanjaji lilipoanza kutekelezwa nchini, mpaka kufikia Machi 4, mwaka huu, zaidi ya watu milioni 2.6 wamepata dozi kamili ya chanjo, huku akisisitiza wananchi kuendelea kuchukua hatua zote za kujikinga kwa kuhakikisha wanapata kwa wakati dozi kamili za UVIKO-19.

Mganga mkuu aliwataka wananchi kuvaa barakoa kwa usahihi na wakati wote wanapokuwa kwenye mikusanyiko na kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono (sanitizer).

Pia aliwataka wananchi kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya endapo watakuwa na dalili za ugonjwa huo na kuendelea kuchukua hatua za kujenga mwili imara kwa kufanya mazoezi na kula vyakula bora.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (kulia), akikabidhi zawadi ya kitabu kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Mipango wa Uganda, Keefa Kiwanuka, wakati kamati hiyo ilipotembelea TRA, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu ukusanyaji kodi. **PICHA: TRA**

# Waiba jeneza msikitini na kutoweka nalo

**Na Haimsi Nasri,** MASASI

WATU wasiojulikana katika Kijiji cha Rivango, Kata ya Mchauru, wilayani Masasi mkoani Mtwara, wamevunja mlango wa msikiti na kuiba jeneza linalotumika kwa ajili ya shughuli za maziko na kutoweka nalo.

Akizungumza na Nipashe jana kijijini hapo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Rivango, Shabani Mohamedi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba tukio hilo limetokea usiku wa Machi 5, usiku wakati waumini wakiwa tayari wameshaondoka baada ya kuswali ibada ya saa mbili usiku.

Alisema kuwa watu hao wasiojulikana walifika katika msikiti huo na kufungua mlango wa msikiti kisha kuingia ndani na kuiba jeneza hilo na kuondoka nalo kusikojulikana.

Mohamedi alisema inaonyesha kuwa watu hao baada ya kubeba jeneza hilo na kukimbia nalo walidondosha baadhi ya vitu vilivyokuwa ndani na kushindwa kuvichukua.

Alisema baadhi ya vitu walivyodondosha ni chaga, shuka ambayo hutumika kufunikia jeneza na mswala.

Mohamedi alisema waumini wa msikiti huo walibaini tukio hilo walipofika asubuhi msikitini na kuona baadhi ya vitu hivyo vikiwa vimetupwa nje ya msikiti huo.

Alisema kutokana na tukio hilo, waumini wa kiislamu wa kata hiyo na maeneo mengine ya jirani wanatarajia kukutana na kufanya dua ya pamoja kuwataka wahusika wa tukio warejeshe jeneza hilo mara moja.

"Tutafanya dua ya pamoja viongozi wote wa dini kuhusu jambo hilo ili matukio haya na mengine maovu ndani ya kata yetu yasiwe yanafanyika tena maana yamezidi kushamiri sana," alisema.

Alisema baada ya viongozi wa dini wa Msikiti huo wa Rivango kuibiwa Jeneza hilo walikutana na kufanya kikao cha pamoja kujadili suala hilo ili kuona namna ya kuwashika wahusika wa tukio hilo.

"Tunaomba ushirikiano kutoka kwa wananchi tuunganishe nguvu zetu kuwasaka waliohusika na kuwafikisha katika vyombo vya sheria ili sheria iweze kuchukua mkondo wake," alisema Mohamedi.

Kwa upande wake, mmoja wa kiongozi wa dini wa kata hiyo ya Rivango, Ahmadi Namkolo, ambaye ni mjumbe wa kamati ya ulamaa BAKWATA, Kata ya Mchauru alisema kuwa waumini wanajiandaa kukutana na kufanya dua ya pamoja kuhusu suala hilo.

Alisema katika kata hiyo kumekuwa na matukio mengi ya kuibiwa vifaa mbalimbali kwenye nyumba za ibada na kwamba kuna haja ya kufanya dua ya kuombea jamii kuacha matukio kama hayo.

Naye Katibu wa BAKWATA Wilaya ya Masasi, Hamisi Baina, alisema amepata taarifa na uongozi wa kata ya Mchauru kuhusu tukio hilo na kuthibitisha kutokea kwa tukio hilo.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER NOTICE**

**INVITATION TO BID: NO. ITB/2022/SUP/006 FOR THE SUPPLY OF REGISTRATION MATERIALS**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for the supply of registration materials.

**2. Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

Kindly download the tender documents in the below link:

**https://drive.google.com/drive/folders/14jB6HPb9tAeOI4MDL4slMAtBRKZO-6ma**

If you fail to access the link, please write to **ndassa@unhcr.org** copy **ishobeza@unhcr.org**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Friday 18th March 2022 at 1800 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Monday 28th March 2022 at 1600hrs EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*



**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala-Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala-Lugala na Nala-Segu kuwa muda wao wa kulipia viwanja hivyo umeisha. Aidha, katika kuwawezesha kukamilisha malipo hayo, amewaongezea muda hadi tarehe 27.03.2022.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, viwanja ambavyo vitakuwa bado vinadaiwa vitarudishwa sokoni ili wateja wengine wavinunue bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji, DODOMA**

21673401

# Mama adaiwa kuua mwanawe kwa sumu

**Na Said Hamdani, LINDI**

WATOTO wawili mkoani Lindi wamefariki dunia katika matukio tofauti, likiwamo la mama mzazi kudaiwa kumnywesha sumu ya kuua magugu kutokana na kinachodaiwa kuchukizwa na kitendo cha mkwe wake kukataa kumchukua mjukuu wake huyo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka wilayani Nachingwe na Ruangwa yalikotokea matukio hayo huku zikithibitishwa na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Foka Dinya, matukio ya vifo vya watoto hao wenye umri wa mwaka mmoja kila mmoja, yalitokea mchana wa Machi tano mwaka huu na usiku wa Machi sita mwaka huu.

Kamanda Dinya aliiambia Nipashe jana kuwa mama wa mtoto aliyedaiwa kunyweshwa sumu, ni mkazi wa Kijiji cha Mchichili, Wilaya ya Ruangwa.

Inadaiwa kuwa mauaji hayo yalifanywa na mama huyo ambaye polisi wameficha jina lake, Machi 5 mwaka huu majira ya saa tano usiku baada ya mama mkwe wake kumkatalia kumpokea mjukuu wake kwa maelezo kwamba bado ni mdogo na anahitaji kunyonya maziwa ya mama yake.

"Mtuhumiwa alimchukua mwanawe na kumpeleka kwa bibi yake, lakini bibi alikataa kumpokea kwa vile alikuwa bado ananyonya," alidai Kamanda Dinya katika mazungumzo na Nipashe kuhusu tukio hilo jana.

Alisema uchunguzi wao wa awali umebaini kitendo cha bibi kukataa kumchukua mjukuu wake, kilisababisha mtuhumiwa ambaye kwa sasa anashikiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano, kuchukua uamuzi wa kumuua mwanawe ilipofika majira ya saa tano usiku.

Kaimu Kamanda huyo alidai kuwa mtuhumiwa alichukua sumu ya kuulia magugu na kumnywesha mtoto huyo na kuukatisha uhai wake.

Kamanda Dinya alisema mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani wakati wowote kujibu shtaka linalomkabili baada ya kukamilika taratibu zote, ikiwa ni pamoja na upelelezi.

Kifungu cha 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinalitaka Jeshi la Polisi ama kumfikisha mahakamani au kumwachia huru mshtakiwa ndani ya saa 24 tangu kukamatwa kwake isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.

Katika tukio la pili, kwenye Kata ya Ugawaji, Tarafa ya Nambambo, Wilaya ya Nachingwea (jina halijatajwa), amefariki dunia kutokana na kinachodaiwa kutumbukia kisimani alipokuwa akicheza na wenzake.

Kamanda Dinya alisema kisima hicho chenye urefu wa futi 12, kilikuwa kimejaa maji na mwili wake ulipoopolewa, ulifanyiwa uchunguzi na wataalamu wa afya kisha kukabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya taratibu za mazishi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (wapili kulia), akikata keki ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni baadhi ya wafanyakazi wanawake wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Video tukio mauaji dada wa Bilionea Msuya yapingwa

**Na Kulwa Mzee**

MAWAKILI wa utetezi katika kesi ya mauaji ya dada wa Bilionea Erasto Msuya, Aneth Msuya, wamepinga kupokelewa kwa mkanda wenye video inayomwonyesha mke wa bilionea huyo, Miriam Mrita, akihojiwa na kuelezea tukio la mauaji kwa madai haina tija kisheria na haiku-wapo katika orodha ya vielelezo.

Hoja hizo za pingamizi ziliwasilishwa na Wakili Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko, jana Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji Edwin Kakolaki, wakati shahidi namba sita, Inspekta Aris-tides Kasigwa, alipoomba kutoa kielelezo cha 'tape'.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Genes Tesha, shahidi huyo alidai yuko Kamisheni ya uchunguzi wa kisayansi katika Makao Makuu ya Polisi, Dar es Sa-laam.

Alidai Agosti 8, mwaka 2016, Mkuu wake wa kazi alimpa barua iliyotoka kwa Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), ili-yokuwa inataka mtaalamu wa picha mna-to na video na alitakiwa kufanya kazi ya kumrekodi mtuhumiwa.

"Alikuja afande David na afande Ju-manne, walitaka niongozane nao Kituo cha Polisi Uwanja wa Ndege, wakasema kuna mtuhumiwa wa kurekodi video.

"Nilienda ofisi ndogo ya Kituo cha Polisi Uwanja Ndege, nikamkuta afande Latifa na mtuhumiwa, afande Jumanne na David walitoka nje, afande Latifa alikuwa anamuhoji mtuhumiwa na mimi nachukua video ya mahojiano.

"Tulienda naye Kigamboni, nilitengeneza CD mbili nikaweka katika bahasha, nikaweka jina na saini yangu," alidai shahidi. Aliomba kutoa bahasha kama kielelezo, haikupingwa na mahakama ilipokea na kuruhusu afungue bahasha hiyo.

Shahidi baada ya kufungua bahasha alitoa 'tape' yenye video ya mahojiano aliyofanya afande Latifa, aliomba kutoa tape hiyo kama kielelezo mahakamani, lakini mawakili wa utetezi walipinga.

Akiwasilisha hoja Wakili Kibatala alidai, wanapinga kupokelewa kwa kielelezo hicho kwa sababu mbalimbali ikiwamo kwamba shahidi amekwenda kinyume na utaratibu wa kutoa kielelezo cha kielektroniki.

Alidai hakuna kiapo kilichowasilishwa kuhusiana na kielelezo hicho na kwamba 'tape' haikuzungumziwa na upande wa mashtaka kama itatolewa kwenye ushahidi wakati wa kusoma maelezo ya mashahidi kwenye mahakama ya chini.

Kibatala alidai upande wa mashtaka unatoa tape hiyo kuonyesha mshtakiwa alikiri makosa ya mauaji, lakini ushahidi huo hauna tija kwa sababu si miongoni mwa ushahidi wa kukiri ulioainishwa kwenye sheria. Wakili Nehemiah alidai shahidi kashindwa kueleza mahakamani vifaa alivyotumia kurekodi vilikuwa vya aina gani ikiwamo kamera iliyotumika.

Mawakili wote waliomba mahakama isipokee kielelezo hicho kwa sababu hizo na kwamba shahidi hana sifa ya kutoa kielelezo hicho.

Akijibu, Wakili Tesha alidai shahidi wake ni sahihi na anayo sifa ya kutoa kielelezo hicho mahakamani.

Alidai si kweli kwamba wakati shahidi anachukua video hiyo alikuwa chini ya uangalizi wa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini.

Wakili Tesha anadai hoja hiyo haina mashiko kwa kuwa shahidi wake alifanya kazi hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Makosa ya Jinai na aliomba kielelezo kipokelewe.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja hizo inatarajia kutoa uamuzi wa kupokea ama kukataa kupokea kielelezo hicho leo.

Katika kesi hiyo ya mauaji washtakiwa ni mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara, Revocatus Muyella.

Kesi ya msingi namba 103/2018, washtakiwa hao wanadaiwa kumuua kwa kukusudia, Aneth Msuya, dada wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Mei 25, mwaka 2016 maeneo ya Kibada Kigamboni, Dar es Salaam.

## KESI YA SABAYA

# Shahidi adai kutohusika kuunda genge la uhalifu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

SHAHIDI wa nne wa utetezi, John Odemba, katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amedai kwamba hakuwahi kuhusika kuunda genge la uhalifu wala kutakatisha fedha Sh. milioni 90.

Alitoa ushahidi huo mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Dk.Patricia Kisinda.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Moses Mahuna, shahidi huyo mwenye umri wa miaka 49, mfanyabiashara na mkazi wa Njiro, jijini Arusha, ambaye ni mshtakiwa wa nne katika kesi hiyo, alidai kwamba anafanya biashara ya nguo za watoto, wanawake na wanaume na amefanya shughuli hiyo kwa muda wa zaidi ya miaka nane.

Alidai amemsikia mfanyabiashara Francis Mroso, wakati akitoa ushahidi mahakamani na ilikuwa mara yake ya kwanza kumfahamu na kumuona. Pia, alidai Januari 22, 2021 aliamka asubuhi na kwenda katika biashara yake hadi usiku majira ya saa 3:00 usiku aliporejea nyumbani kwake.

Kadhalika alisema hakuwahi kukamatwa bali Mei 20 mwaka 2021 alipigiwa simu na kutakiwa kufika kituo cha polisi na alipofika aliulizwa kama anamfahamu Sabaya au kama aliwahi kuwasiliana naye na baada ya hapo walimwachia.

Maofisa hao, walimweleza kwamba endapo asingetoa ushirikiano wangempoteza na kwamba alibaki na msimamo wake wa kutokusema uongo. Alidai kwamba alishikiliwa kwa siku 14 mahabusu ya TAKUKURU na kwa wakati wote alipigwa na baridi akiwa kwenye sakafu bila ya kupewa fursa ya kuzungumza na ndugu zake wala ya kufikishwa mahakamani.

Pia, hakuwahi kushiriki kuunda genge la uhalifu na ndiyo kwa mara ya kwanza amesikia shtaka hilo.

Kadhalika alidai kwamba hakuwahi kutakatisha Sh. milioni 90 kwa kuwa hakuma ushahidi wowote uliotolewa mahakamani kuthibitisha kwamba alihusika kutakatisha kiasi hicho cha fedha.

Vilevile alidai kwamba hafahamu amehusishwaje na watu wenye sura za kutisha kama ilivyodaiwa na Mroso kwenye maelezo yake aliyoandika kituo cha polisi na alipomtambua mahakamani alipomshika wakati akitoa ushahidi.

Pia, Julai 16, mwaka 2021 akiwa katika Gereza la Kisongo, majira ya saa 4:00 waliitwa na ofisa wa Magereza na kuelezwa kuwa maofisa wa nne wa TAKUKURU wanataka kuzungumza nao.

Naye shahidi wa pili wa utetezi, Enock Togolani, katika kesi hiyo alidai kwamba hakuwahi kukamatwa na maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), bali alipigiwa simu akitakiwa kufika katika ofisi za taasisi hiyo.

Akihojiwa na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Jacopiyo Richard, alidai kwamba hakukamatwa na maofisa wa taasisi hiyo bali alipigiwa simu.

# Mabula aanika mafanikio ardhi mwaka mmoja uongozi wa Samia

Na Munir Shemweta

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akitimiza mwaka mmoja Machi 19, mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameanika mafanikio ya mwaka mmoja katika sekta ya ardhi.

Dk. Mabula amesema sekta hiyo imepiga hatua kubwa katika masuala mbalimbali ikiwamo usajili wa hati na kuongeza kasi ya upimaji ardhi nchini huku akibainisha kuwa serikali ya Rais Samia imeiwezesha wizara kupitia miradi mbalimbali kuhakikisha inapanga, inapima na kumilikisha ardhi.

Akizungumzia mafanikio hayo jana, Dk. Mabula alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wizara ilipatiwa Sh. bilioni 50 kama mkopo kwa ajili ya Program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika halmashauri mbalimbali nchini.

Pia alisema katika kipindi hicho, serikali iliiwezesha wizara kupatiwa Sh. bilioni 345 na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha milki za ardhi nchini.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na kusajiliwa hatimiliki 41,533 na hati za sehemu ya jengo 161 sambamba na kusajiliwa hatimiliki 3,735 za kielektroniki kupitia mfumo wa ILMIS.

Aidha, Dk. Mabula alibainisha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja, Wizara yake ilikamilisha kazi mbalimbali za uthamini ikiwamo uthamini wa mali za wananchi kwenye ujenzi wa barabara ya pete jijini Dodoma yenye thamani ya Sh. bilioni 12.76 na ile ya kijiji cha Fella wilayani Misungwi kupisha ujenzi wa kambi ya mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

"Pamoja na kazi kubwa iliyofanyika kwenye suala la utathmini, wizara imekamilisha pia majedwali ya fidia ya mali za wananchi 1,525 katika mkuza wenye urefu wa kilomita 89 ambapo Sh. 3, 818, 123, 062 zitalipwa kama fidia kwa waathirika," alisema Dk. Mabula.

Pia alisema wizara ilitatua migogoro ya ardhi 745 katika mikoa na halmashauri mbalimbali nchini kupitia programu ya Funguka kwa Waziri huku ikifanikiwa kukusanya Sh. 119, 501,946.6 kupitia kodi ya pango la ardhi.

Kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Dk. Mabula alisema serikali imeliwezesha shirika hilo kupata fedha za kukamilisha miradi yake mbalimbali iliyosimama pamoja na ile ya kimkakati.

## Kampeni kuhamasisha bima NMB yazinduliwa

Na Mwandishi Wetu

KAMPENI maalum yenye lengo la kutoa hamasa na elimu juu ya umuhimu kwa bima kwa Watanzania imezinduliwa.

Kampeni hiyo iliyoitwa "Umebima? Siyo ngumu kihivyo" ilizinduliwa jana na Benki ya NMB katika Soko la Karume jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na kampuni 10 za bima, huduma inayopatikana kupitia matawi ya benki hiyo kote nchini.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema licha ya umuhimu wake kwa maisha ya Watanzania na katika shughuli za kila siku, bado mwitikio wa watu kukata bima umekuwa mdogo sana.

"Pamoja na elimu kutolewa, bado idadi ya watu wanaoweka bima ni ndogo sana, ambapo ni asilimia 15 tu ya Watanzania ndio wanaotumia huduma za bima, idadi hii bado ni ndogo sana," alisema Mponzi.

"Lengo la Benki ya NMB kupitia kampeni hii ni kueneza elimu na hamasa juu ya uwekaji wa bima ili idadi hii ya Watanzania wenye bima iongezeke kutoka asilimia 15 mpaka 50 ya Watanzania ifikapo mwaka 2030."

"Kwa sababu za kijiografia, tunatambua kuwa kampuni hizi za bima hazijafikia maeneo yote nchini, lakini kwa kuwa Benki ya NMB imetapakaa nchi nzima na ina matawi katika wilaya zote nchini, tumeona ni vyema kushirikiana na nazo kuuza bima hizi katika kila tawi la benki yetu. Hivyo ukifika katika tawi lolote la NMB hapa nchini utaweza kununua bima yoyote uitakayo, iwe bima ya afya, Maisha, chombo au yoyote ile," alisisitiza.

Mkuu wa Idara ya Bima wa Benki ya NMB, Martine Massawe, alisema kuwa kampeni hiyo haijazinduliwa Dar es Salaam tu, bali na katika mikoa mbalimbali nchini huku lengo likiwa kufika katika mikoa yote ya Tanzania kueneza elimu hiyo muhimu ya bima.

Uzinduzi huo pia ulihudhuriwa na Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, utafiti na maendeleo ya masoko wa Tume ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Zakaria Muyengi na waathirika wa moto ulioteketeza soko la Karume, lakini kwa kupitia bima walizokata na Kampuni ya Reliance Insurance kupitia Benki ya NMB walilipwa hasara yao na sasa wanaendelea vyema na biashara zao.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendelee kuwatambua, kuwajali na kuwawezesha wenye mahitaji maalum

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi alieleza alichozungumza faragha na mwanafunzi, Emanuel Mzena, akiahidi kutimiza ndoto zake ikiwamo kumsomesha nje ya nchi na kumfungulia taasisi kwa ajili ya kuwasemea watoto wenye mahitaji maalum.

Aidha, akihutubia wanafunzi wa Shule ya Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam, alisema serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kupata elimu bora.

Alisema jitihada hizo ni kuhakikisha kwamba elimu jumuishi kuanzia awali, msingi, sekondari na vyuo inakuwapo, na lengo kubwa ni kutekeleza azimio namba 4 katika maazimio ya mendeleo endelevu.

Pia awapongeza walimu kwa kazi nzuri huku ikiwataka kuendelea kufanyakazi kwa bidii, ili kuhakikisha wenye mahitaji maalum wanapata elimu sahihi.

Changamoto za wenye ulemavu ni nyingi kuanzia kwenye maumbile yao, ndani ya familia na kwenye jamii kwa ujumla kwa kuwa wanashindwa kufikia ndoto zao kama watu wengine.

Baadhi ya familia huwakataa wenye ulemavu, kuwatelekeza na wengine kuwaficha kwa kuogopa kuchekwa au kujulikana na jamii kuwa wana watu wenye hali hiyo.

Baadhi bila woga wanawatumia kama omba omba kwenye mitaa mbalimbali wakiwaendesha kwenye viti mwendo kuwa hao wanahitaji msaada kwa wapita njia, lakini kiuhalisia fedha hizo huelekezwa kwa wasio na ulemavu huku wahusika wakiumia.

Pia, baadhi ya maeneo miundombinu muhimu kwa ajili yao haijawekwa, jambo linalowafanya washindwe kupata elimu au huduma muhimu za kijamii kama wengine.

Kutokana na mazingira hasa ya milimani na hali duni za familia zao, wengine wameshindwa kwenda shuleni au kupata huduma nyingine, jambo ambalo linahitaji ushirikiano wa jamii kwa kuwatambua na kuwasaidia.

Jitihada za kuwatambua zimeendelea na kuwasaidia, lakini bado kazi ni kubwa kwa kuwa mazingira waliyoko ni magumu, yanawanyima kupata fursa muhimu za maisha yao.

Lazima kuendelea kuwasaidia wenye mahitaji maalum kwa kuwahakikisha miundombinu muhimu inakuwapo, huduma nzuri za afya na vifaa vya kujifunzia na kusomea.

Mathalani, bado kuna vikwazo vya kupata vitabu vya nukta nundu, karatasi na machapisho mengine muhimu ya kufikisha elimu mbalimbali kwao, mfano kwa taarifa za serikali, mashirika na taasisi mbalimbali.

Wengi bado wanalilia kuwapo kwa fimbo maalum za kuwaongoza, viti mwendo, nukta nundu na watafsiri wa lugha za alama maeneo mbalimbali ili kuhakikisha elimu jumuishi inawafikia.

Upo umuhimu kuendelea kusaidia makundi haya bila kuchoka, kwa kuwa ni wachache kwenye jamii, lazima kubadili mtazamo wa jamii kuwa wanaweza kufanya mambo ambayo hata wasio na ulemavu wanafanya, lakini kila mmoja kukumbuka kuwa ni mlemavu mtarajiwa.

Jitihada za serikali zimekuwapo, lakini lazima ziendelee kuhakikisha kuwa kila mwenye mahitaji maalum anapata huduma zote muhimu kwa faida ya wote.

Ni matarajio yetu kwamba kauli ya Rais Samia inaakisi utashi wake binafsi na wa serikali yake katika kuwajali na kutaka kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum, hivyo jamii nzima iwajibike kuhakikisha hilo linatekelezwa.

Kwa kufanya hivyo jamii yetu itakuwa imetimiza wajibu wake katika kujali na kuheshimu haki za binadamu. Kwa kuwa kila binadamu anastahili haki zote zikiwamo za kijamii, kiraia, kiuchumi na kiutamaduni kama inavyoainishwa na Tamko la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948 la Haki za Binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mapendekezo ya LHRC kuhusu usawa wa kijinsia ni ya muhimu

**MAADHIMISHO** ya Siku ya Wanawake Duniani yamekamilika jana, Zanzibar, huku kukiwa na matamko na mapendekezo mbalimbali yanayotolewa na wadau wa haki za wanawake yanayolenga kuimarisha usawa wa kijinsia nchini.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni miongoni mwa wadau wakubwa wa haki za binadamu, ambacho kimekuja na mapendekezo yenye lengo la kuimarisha usawa huo na kukomesha ukatili wa kijinsia.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia na haki za wanawake, kuimarisha huduma za jamii na kusaidia wanawake wanapopata changamoto za ukatili.

Mengine ni wanawake kutumia fursa zilizoko kujiendeleza na kuhakikisha wanapata elimu ya kutosha inayohusiana na masuala yanayohusu ili waendelee kuwa chachu ya kukemea mfumo unaowakandamiza.

Kwenye ukatili wa kijinsia, LHRC inapendekeza kutengenezwa sheria mahususi ya ukatili wa kijinsia ili kulinda wanawake na jamii kwa ujumla dhidi ya vitendo vya ukatili, kurekebisha sheria kandamizi zinazoendelea kuathiri wanawake.

Aidha, jamii kutofumbia macho vitendo vyovyote vya ukatili na kutoa taarifa pale mtu anapofanyiwa vitendo vya ukatili, ni pendekezo lingine ambalo limo kwenye tamko lililotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Anna Henga.

Ni katika mkutano wake na wanahabari alipokuwa akitoa tamko la kituo hicho katika kilele cha maadhimisho ya siku hiyo, akisema kwamba bado kuna vikwazo vingi ambavyo wanawake wanakumbana navyo.

Aidha, pamoja na kuwapo kwa hatua zilizofikiwa kwenye suala la usawa wa kijinsia, kuna changamoto hasa kukithiri kwa ukatili dhidi ya wanawake ambazo zinaendelea kutokea kila kukicha.

Naamini kuwa, iwapo mapendekezo ya kituo hicho yatazingatiwa na kila mmoja, yanaweza kuimarisha usawa wa kijinsia, lakini pia kupunguza vitendo vya ukatili ndani ya jamii ambavyo kwa namna moja au nyingine vinahatarisha maisha ya wanawake na watoto.

Henga anakiri kuwapo kwa mafanikio katika kuwajengea wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi zikiwamo ambazo hazikuwahi kushikiliwa na mwanamke kama Waziri wa Ulinzi, Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu na Katibu wa Bunge.

Anataja baadhi ya nafasi hizo za uongozi kuwa Baraza la Mawaziri, kuongezeka kwa wanawake kutoka mawaziri wanne hadi kufikia tisa dhidi ya 16, mabalozi wanawake tisa dhidi ya 33, wakuu wa mikoa sita dhidi ya 20, wakuu wa wilaya 40 dhidi ya 101, ni mafanikio.

Kwa maelezo yake, ni wazi kwamba, safari kufikia asilimia 50 kwa 50 inaendelea vizuri lengo likiwa kumnyanyua mwanamke, kwa mazingira hayo ni vyema wale wanaopata nafasi hizo wakitumia inavyotakiwa.

Ndani ya harakati hizo za kutafuta usawa wa kijinsia ni vyema pia jamii kushiriki katika vita ya kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vinarudisha nyuma maendeleo ya mwanamke.

Kwa mfano, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi Mtendaji huyo anasema, mwaka 2020 kituo hicho kiliripoti matukio 7,263 ya ubakaji na mengine 26,544 ya ukatilki dhidi ya wanawake.

Nionavyo ni kwamba, vita dhidi ya vitendo hivyo, si vya serikali na wadau wake, bali ni kila mmoja kwa nafasi yake hasa kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola anapoona dalili au kuwapo kuwa na tukio la ukatili wa kijinsia.

Tanzania inayoamini na kusimamia usawa wa kijinsia inawezekana kama ambavyo Henga anasema, kuwa haki za wanawake ni haki za binadamu, hivyo vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi yao havipaswi kufumbiwa macho.

Pamoja na hayo, jambo lingine la muhimu katika kufanikisha vita hiyo, ni kuendelea kutolewa kwa elimu katika jamii kuhusu haki za binadamu ili kusaidia kutokomeza ukatili wa aina zote.

HABARI KITAIFA




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (kushoto), akizindua rasmi Bima mpya ya UMEBIMA, katika viwanja vya Soko la Karume, Ilala jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life, Hellen Mzela (kulia) ni Mkuu wa Idara ya Bima NMB, Martine Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafanya mafunzo kujenga uelewa kuhusu uchumi wa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendesha mafunzo ya kujenga uelewa kwa viongozi wa serikali kuhusu uchumi wa kidijitali

Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, alifungua mafunzo ya kujenga uelewa kwa viongozi wa serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar kuhusu uchumi wa kidijitali katika ukumbi wa Hoteli ya Marijana, Pwani ya Kichangani, Zanzibar. Mafunzo hayo ni ya siku nne na yalianza rasmi jana.

Balozi Katanga alizipongeza uongozi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kuandaa mafunzo hayo kwa viongozi hao kwa kuwakutanisha pamoja.

"Mmefanya jambo jema leo (jana) kwa kuwakutanisha viongozi hawa wenye maarifa, ujuzi na uelewa mbalimbali kwa lengo la kuwaongezea maarifa kuhusu ujenzi wa uchumi wa kidijitali," alisema.

Balozi Katanga alisema suala la uchumi wa kidjitali ni mtambuka, hivyo aliwataka viongozi wenye nafasi ya kufanya uamuzi katika masuala ya kisera na kiutendaji ndani ya serikali kutumia fursa ya mafunzo hayo kujenga uelewa kuhusu mabadiliko hayo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) yanaliwezesha taifa letu kukuza uchumi.

Aliitaka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuchukua jukumu la kuendelea kuwa wazazi kwa kukuza sekta ya mawasiliano baina ya serikali; sekta binafsi na wananchi na kubadilika kwa haraka kuendana na maendeleo ya sekta hiyo ili kwenda sambamba na mabadiliko haya na kwenda na wakati hatimaye kupeleka nchi kwenye kiwango cha juu.

Katika kufanikisha hayo, alisema mambo ya msingi ni kufungua fursa mpya, kuongeza mapato ya kodi, mifumo ya kiutendaji, upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi, huduma za utalii na kuitangaza nchi kimataifa; kufanikisha ongezeko la huduma za intaneti na upatikanaji wa ajira.

Sambamba na hayo alisema mfumo huo mpya unapaswa kuleta mabadiliko kwenye nchi ikiwa ni pamoja na kuongeza wabobezi wenye ujuzi; kuendeleza na kupanua miundombinu ya kimkakati ya TEHAMA na anwani za makazi pamoja na kutafuta masoko.

"Ni imani yangu kuwa mafunzo haya yataliwezesha taifa kunufaika na kwenda kasi na ukuaji wa TEHAMA duniani ikiwa ni pamoja na kuwa na mtandao wenye kasi kubwa; usalama wa mtandao; kupatikana kwa bidhaa na huduma," alisema.

Naye Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema mafunzo hayo yatafanyika kwa makundi mbalimbali ili viongozi wengine wapate mafunzo haya na kunufaika nayo.

Alisema viongozi ndio wanaoshika usukani wa kuendehsa nchi, hivyo wakielewa watandesha vyema taasisi za serikali ili kuendana na ukuaji wa uchumi na uchumi wa kidijitali ili wananchi na taifa kunufaika na maendeleo ya TEHAMA nchini kuelekea Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ambayo Tanzania imeamua kujikita kujenga uchumi wa kisasa wa kidijitali kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo 2025.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi alisema anaamini kuwa baada ya mafunzo hayo, serikali itabadilisha kabisa namna ya utendaji kazi kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kukuza, kuendeleza na kuongeza matumizi ya uchumi wa kidijitali.

Pia alisema Serikali itatumia fursa hiyo ya kidijitali kuhakikisha sekta mbalimbali zinatumia uchumi wa kidijitali ili kuwezesha mwingiliano wa masuala ya TEHAMA katika kunufaisha taifa kwa kuwa serikali inaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi ambapo majina ya mitaa/barabara na namba za nyumba zitawawezesha wananchi kunufaika na uchumi wa kidijitali kwa kuwa watatambulika; kufahamika na kupata huduma mahali walipo.

# Waziri aonya uvamizi wa maeneo Chalinze

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema hakuna nafasi itakayotolewa kwa wanaoingia kwenye maeneo ya watu bila kufuata sheria, wakisubiri huruma ya serikali.

Amesema serikali haiko tayari kuendelea kuwavumilia watu hao ambao wamekuwa wakisababisha migogoro ya mara kwa mara na kurudisha nyuma maendeleo.

Ridhiwani alitoa angalizo hilo alipozungumza na wananchi katika Kata ya Msoga, akibainisha kuwa wapo watu maarufu kwa jina la 'tegesha' ambao wamekuwa wakiingia kwenye maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili baadaye walipwe fidia.

Ridhiwani ambaye pia ni Mbunge wa Chalinze, aliwataka wenyeviti na watendaji kuanzia ngazi ya vijiji, kusimamia sheria na taratibu katika kuwakaribisha wageni kwenye maeneo yao.

"Msiishie kukaribisha watu wanaofuga, ulizeni na idadi ya mifugo waliyonayo. Rais Samia Suluhu Hassan anataka tusimamie haki, tutafanya hivyo kwa kusimamia sheria," alisema.

Ridhiwani alisema vijiji na wananchi wakipewa ardhi yao, kutasaidia kupunguza migogoro isiyoisha ambayo imekuwa ikileta uhasama kwa wananchi wenyewe kwa wenyewe na kusimamisha shughuli za maendeleo.

"Nimeshuhudia watu wanakuwa walemavu, nimezika na kushuhudia misiba mingi inayotokana na migogoro, hatuwezi kukubali hali hii iendelee. Ifikie wakati wa kuimaliza na watu wapimiwe maeneo yao, mipaka iainishwe," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, aliwataka wananchi kuacha kuogopana na badala yake kuwafichua wanaohusika kuchangia uwapo wa migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

Alisema kumekuwa kukifanyika mikutano ya mara kwa mara ambayo ililenga kutatua migogoro ya ardhi lakini haijaleta matokeo chanya kutokana na baadhi ya wananchi kuwaficha wanaohusika na kusababisha migogoro hiyo kuendelea.

"Ndugu yangu naibu waziri tumekuja kwenye mikutano mara kwa mara kuliongelea suala hili na hawa wananchi lakini bado wanaendelea kulalamika kutomalizika kwa tatizo la kulishiwa mazao yao, hili sasa liko huku chini, tutarudi tena sisi viongozi wa halmashauri tuzungumze nao wawafichue wanaohusika na sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri hiyo, Musa Kichumu, aliahidi kushirikiana na wananchi kumaliza migogoro iliyopo kwa kufanya nao mikutano ambayo itahusisha timu ya idara yake ya ardhi.

Baadhi ya wakazi wa vijiji vya Kata ya Msoga walieleza namna wanavyokabiliwa na kero ya mifugo kuharibu mazao yao mara kwa mara na kuwasabishia hasara.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MKUTANO WA WADAU WANAOTEKELEZA MIRADI MBALIMBALI KATIKA SEKTA YA MAJI**

Kuelekea Wiki ya Maji 2022, Wizara ya Maji inawaalika katika mkutano wadau wanaotekeleza miradi mbalimbali katika sekta ya maji, wakiwemo Wakandarasi, Wahandisi washauri, wamiliki wa viwanda vinavyozalisha vifaa vya ujenzi wa miradi ya maji, wasambazaji wa vifaa vya ujenzi wa miradi ya maji, wasambazaji wa madawa ya kutibu maji na makampuni ya utafiti na uchimbaji wa visima.

Maudhui ya kikao ni kushauri na kutoa mapendekezo ya kuboresha ushirikiano baina ya Wizara na wadau wa lengo la kuongeza kasi ujenzi wa miradi ya maji na masuala yanayohusiana na Sekta ya Maji hapa nchini,. Mkutano utafanyika Tarehe 10 Machi, 2022.

**ENEO:** Ukumbi wa St. Gaspar, Jijini Dodoma
Mkutano utaanza saa **02:30 (saa mbili nanusu asubuhi)**

Wadau wote mnaalikwa, tafadhali thibitisha ushiriki wako kwa kutuma barua pepe kwa anuani ifuatayo; **tumaini.mwamyala@maji.go.tz** au ujumbe mfupi kwenye namba **0754287683**

**Imetolewa na;**
**KATIBU MKUU**
**Wizara ya Maji**

216737502

# Tanzania mwenyeji katika mkutano wa utalii duniani

**Na Mwandishi Wetu,**
HISPANIA

TANZANIA imetia rasmi saini mkataba wa kukubali kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa utalii wa 65 wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Utalii Duniani (UNWTO), unaotarajiwa kufanyika Oktoba 5 hadi 7, mwaka huu, jijini Arusha.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesaini mkataba huo mbele ya Katibu Mkuu wa UNWTO, Zurab Pololikashvil, Makao Makuu ya Shirika hilo jijini Madrid, nchini Hispania.

Mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na mawaziri wote wa utalii wa Bara la Afrika pamoja, wabobezi wa kutangaza utalii na wataalamu wa masuala ya utalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

Akizungumza baada ya hafla ya utiaji saini, Waziri Ndumbaro alisema mkutano huo ni fursa kwa wadau wa utalii nchini Tanzania kujifunza na kubadilishana uzoefu mkubwa wa kuendesha sekta ya utalii hususani katika kipindi hiki ambacho sekta ya utalii imeanza kuimarika baada ya kuathiriwa na janga la UVIKO-19.

"Tumepewa heshima kubwa ya kuwa wenyeji wa mkutano huu ambao naamini utafungua milango ya vivutio vyetu vya utalii kujulikana duniani kote," alisema Dk. Ndumbaro.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa UNWTO, Zurab Pololikashvil, alisema ataendelea kushirikiana na Tanzania kuhakikisha inaendelea kufanya vizuri katika masuala ya utalii huku akiahidi kuipa kipaumbele katika miradi mingi inayofadhiliwa na Shirika hilo.

"Nimekuwa nikipata ushirikiano wa kutosha kutoka Tanzania kupitia Waziri Dk. Ndumbaro, utiaji saini wa leo wa kuwa Mwenyeji wa mkutano huu ni mwanzo tu wa kuhakikisha Tanzania inafanya vizuri katika masuala ya utalii," alisisitiza Katibu Mkuu huyo.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akitiliana saini mkataba na Katibu Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya utalii duniani (UNWTO), Zurab Pololikashvil, mjini Madrid, nchini Uhispania, Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa 65 wa utalii, unaotarajiwa kufanyika Oktoba 5 hadi 7 mwaka huu, jijini Arusha. **PICHA: WMU**

# Mabasi mapya 95 mwendokasi yaja

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umesema mwaka huu utaongeza mabasi mengine mapya 95 ikiwa ni sehemu ya hatua za kupunguza msongamano wa abiria kwenye vituo vya mabasi hayo.

Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Dk. Edwin Mhede, alibainisha hayo jana wakati akifungua mafunzo kuhusu mipango ya mitaa kwa Jiji la Dar es Salaam.

Alisema wakala ulijitahidi kuongeza mabasi 70 hivi karibuni kwa ajili ya kupunguza msongamano huo lakini kutokana na wananchi wengi kuchangamkia usafiri huo, mahitaji yanaendelea kuongezeka.

Alisema zamani abiria alilazimika kusubiri basi kwa dakika 30 lakini walipoongeza mabasi 70, muda huo ulipungua na kufikia dakika tano na kwamba mpango uliopo unalenga kuondoa hata hizo dakika tano ili abiria akifika tu apande basi na kwenda anakotaka.

"Kabla ya mwisho wa mwaka huu tunakusudia kuongeza mabasi mengine mapya 95 na tunaamini kwa kufanya hivi tutaondoa kabisa muda wa kusubiri kwa sababu maana ya kuwapo kwa mabasi haya ni watu kuwahi makazini," alisema

Dk. Mhede alisema ujio wa mabasi hayo pia utapunguza kawaida ya watu kukimbizana kupanda mabasi, hali ambayo imekuwa ikisababisha ajali kwenye vituo hivyo kutokana na watu kukanyagana au kugongwa na mabasi.

Aliwaomba wananchi kuacha tabia ya kukatisha kwenye njia za DART kwa kuwa si salama kwao na kwa mabasi, akionya kuwa wananchi wengi wamekuwa wakipata majeraha wanapokatisha kwenye njia hizo.

"Hakuna haja ya kukimbilia basi, ukakatisha njia ya UDART uwezekano wa kugongwa ni mkubwa. Sasa ni muhimu ukazingatia usalama wako kwanza kabla ya kuchukua uamuzi wa kukatisha kwenye njia hizo," alionya Dk. Mhede

Kiongozi huyo pia alisema wakazi wa Kigamboni wajiandae kupokea huduma hiyo kwa kuwa fedha za kujenga mradi huo kuelekea maeneo yao zimeshapatikana na kinachosubiriwa ni utekelezaji wa mradi.

Alisema ujenzi wa DART kuelekea Kigamboni utafanywa kwenye awamu ya tano, akidokeza kuwa ziara za Rais Samia Suluhu Hassan nje ya nchi zimefanikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia mradi huo kwa awamu ya tano.

Alisema ujenzi wa mradi huo kuelekea Kigamboni utapitia kwenye Daraja la Nyerere na maandalizi kwa ajili ya utekelezaji wake yanaendelea vizuri.

DART kwa kushirikiana na Shirika la Makazi Duniani (UN- HABITAT) na Taasisi ya Usafiri na Maendeleo (ITDP), wameandaa mafunzo hayo ya siku mbili kwa ajili ya watumishi wanaohusika na mipango miji na mitaa ya Jiji la Dar es Salaam.

# Teknolojia mpya kusaidia wafugaji

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema wanatarajia kusambaza teknolojia mpya ya Juncao kwa wafugaji, ili kukabiliana na tatizo la mifugo kufa kwa kukosa chakula.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano kwa ajili ya kujadiliana teknolojia ya Juncao itakayoanza kutumiwa kwa wafugaji nchini.

Alisema wameamua itumike nchini kwa kuwa wanataka kuziba pengo la malisho ya mifugo nchini na wameomba msaada wa China ili kuwasaidia kuitawanya kwa wafugaji, taasisi na vituo vya mifugo nchini.

Ndaki alisema wameiomba Serikali ya China iwapatie uthibitisho wao kwa kuwa mazungumzo yalishafikia hatua nzuri.

"Siku ya leo tumetumia nafasi ya tukio hili kuiomba Serikali ya China itupatie msaada kwa sababu huu ndiyo wakati wake kwa Tanzania teknolojia ya Juncao itakapoanza kuitumia itatusaidia kwa upande wa wafugaji kwa sababu tunajua mabadiliko ya hali ya hewa yaliathiri upatikanaji wa malisho na vyakula vya mifugo hapa nchini," alisema waziri.

Alisema anakumbuka mwaka jana kulitokea janga kwenye baadhi ya maeneo, mifugo ikafa tatizo kubwa lilikuwa ni malisho pamoja na maji.

"Sisi kama nchi teknolojia hii ya malisho ya Juncao itatusaidia tutakapoisambaza kwa wafugaji wetu kwa sababu inafaa kulimwa katika maeneo yote haijalishi ni ardhi yenye ukame ama inayopata maji kiasi gani malisho haya yanaota itatusaidia kwa wafugaji wetu," alisema Waziri.

Waziri alisema teknlojia hiyo itawasaidia kuongeza uzalishaji wa malisho na kuongeza ubora wa mifugo yao na kupata kipato kikubwa zaidi.

Waziri alisema kikao cha jana ni kwa ajili ya kujadili teknlojia ya malisho iitwayo Juncao ambayo asili yake ni nchini China.

"Kikao hicho tumeangalia matumizi ya teknolojia hii na mafanikio yake katika maendeleo ya ufugaji au ya sekta ya mifugo kwa ujumla wake kwa Tanzania, kwa hiyo washiriki watapata nafasi ya kufahamu vizuri juu ya matumizi ya teknolojia hiyo."

Alisema washiriki wataelewa kwa upana ni namna gani inavyositawishwa, kuboresha ikitumiwa na mifugo, kuboresha uzalishaji ama kuongeza tija kwa wafugaji wa nchini.

Aidha, alisema baada ya kukamilika kwa kikao hicho mchakato wa kupata kibali kutoka serikali ya China utaendelea na kwamba ndani ya mwezi mmoja ujao utakamilika.

Ndaki alisema mchakato huo utakapokamilika wataanza kutoa elimu ya ufahamu kuhusiana na teknolojia hiyo kwa wadau wote wanaohusika, vyuo vikuu na taasisi mbalimbali za serikali na baada ya hapo watakwenda kwa wafugaji.

Aidha, alisema idadi ya mifugo iliyopo nchini ni milioni 67 wakiwamo mbuzi, ng'ombe, kondoo na punda.

Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji wa Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Asimwe Rwiguza, alisema wamekutana kupata utaalamu ili kuona ni namna gani teknolojia hiyo itakavyokwenda kuisaidia Tanzania hasa kwa upande wa uzalishaji wa malisho na uyoga.

"Juncao ni aina ya malisho ya nyasi ambazo zinatumika kwa mifugo na yamefanyiwa utafiti na wenzetu kule China na yameonekana yanakuwa haraka na pia kiwango kikubwa cha protini. Tayari tumejaribu kuyapanda malisho hayo katika shamba letu tumeona malisho hayo yanazalisha kwa wingi shina moja linatoa matawi mengi," alisema Dk. Rwiguza.

## Usawa haki kijinsia wahamasishwa SBL

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema inaendelea kuonyesha njia kwenye masuala ya kijinsia kwa kutoa fursa sawa kwa wanawake kwenye maeneo mbalimbali kama ajira, elimu na mapinduzi ya kilimo.

Napenda kusisitiza kuwa usawa siyo suala la wanawake, ni suala la kibiashara. Biashara yenye usawa ni biashara wezeshi. Usawa wa kijinsia ni muhimu kwa uchumi na jamii kusonga mbele," alisema Mark Ocitti, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2022.

Mkurugenzi huyo alisema kila mtu ana wajibu wa kusaidia kuwepo kwa usawa wa kijinsia.

"Wote tunawajibika kwa mawazo na matendo yetu kila siku. Tukiamua kupinga ubaguzi wa kijinsia tunaweza na tukafurahia kwa pamoja mafanikio ya wanawake,"alisema.

Mark alisema SBL katika programu zake inahakikisha kuwa ujumuishi wa makundi mbalimbali unakuwepo, na kutolea mfano katika programu yao ya ufadhili wa masomo ya kilimo inayojulikana kama Kilimo Viwanda ambayo imefadhili wanafunzi 200 mpaka hivi sasa. "Tumehakikisha kuwa uwakilishi wa nusu kwa nusu kati ya wanaume na wanawake unakuwepo," alisema.

Anasema pia SBL inaendesha programu ya STEM ambayo huwachukua kutoka vyuoni vijana wa kike wanaofanya vizuri katika fani za Sayansi, Teknolojia pamoja na Hisabati na kuwapa fursa ya kujifunza kwa vitendo kwa muda wa mwaka mmoja katika viwanda vyake.

"Tangu tuanzishe programu hii mwaka 2020, vijana wengi wa kile wameweza kupata fursa ya kujifunza kwa vitendo katika idara zetu mbali mbali. Lengo letu ni kuona mtoito wa kike anakuwa sehemu ya maendeleo y sayansi kwa kunufuaika kwa moja kwa moja na fursa mbali mbali," alisema.

Mark alisema SBL kupitia kampuni yake mama ya Diageo imekuwa ikihamasisha ujumuifu wa makundi mbalimbali katika shughuli zake ikilenga kuwa na uwakilishi wa nusu kwa nusu kati ya wanawake na wanaume kufikia mwaka 2030.

**"Wote tunawajibika kwa mawazo na matendo yetu kila siku. Tukiamua kupinga ubaguzi wa kijinsia tunaweza na tukafurahia kwa pamoja mafanikio ya wanawake,"alisema.**

# Polisi kufuatilia biashara haramu ya kutumikisha wenye ulemavu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro limejipanga kufuatilia mtandao wa watu wanaoendesha biashara haramu ya kuwatumikisha watoto wenye ulemavu, kuwatembeza mitaani kuomba fedha na kujipatia kipato kisicho halali.

Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Fortunatus Musilim, alisema hayo mjini hapa kwenye hafla ya wanawake wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) wa mkoa huo.

Alisema, jeshi hilo lina taarifa za kuwapo watu ama mtandao wa watu unao watumia vibaya watoto wenye ulemavu kuwapitisha mitaani wakiomba fedha jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Kamanda Musilim alisema kwa sasa tatizo hilo limekuwa kubwa, lipo ndani ya mkoa huo na watu wanawatumia watoto wenye ulemavu kuwa ni sehemu ya biashara wakiwapandisha kwenye baiskeli zao kupita mitaani na maeneo mbalimbali kujipatia kipato.

"Tumeanza kulifanyia kazi hilo tatizo ili kuweza kuhakikisha watoto hawa wenye ulemavu wasiweze kutumika kuwa ni sehemu ya vyanzo vyao vya mapato," alisema Musilim.

Pia, alisema kama ni suala la misaada kwa watoto hao inapaswa kupitia katika utaratibu unaokubalika badala ya kuwatembeza watoto hao na kuwafanya kama kitega uchumi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wazazi na walezi wenye watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi mkoa wa Morogoro (ASABHT), Korumba Mbiki, alisema mkoa una watoto wenye ulemavu huo wapatao 287 kati yao wa kiume ni 159 na wa kike ni 128.

Kwa upande wake Mganga wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Isabela Shija, alisema kila mwezi wastani wa watoto wawili hadi watatu wanazaliwa wakiwa wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Dk. Shija ambaye anasimamia matibabu yao aliutaja mgogo wazi (Spina Bifida) ni ulemavu ambao hutokea mapema katika wiki tatu za mwanzo za ujauzito.

Alisema sababu ya tatizo hilo bado haijajulikana, lakini wataalamu wanaeleza ya kwamba kwa asilimia 80 husababishwa na upungufu wa vitamini ya Folic Acid kwa mama kabla na wakati wa kujifungua.

Kuhusu kichwa kikubwa (Hydrocephalus), Dk. Shija alisema ni ulemavu ambao mtoto anaweza akazaliwa nao, au kupata baada ya kuzaliwa, husababishwa na kuziba kwa njia za maji zilizomo kichwani kwa sababu ya maambukizi, upungufu wa folic acid, ajali au maumbile.

Dk. Shija alisema, ili kuzuia kujitokeza kwa magonjwa hayo amewashauri wanawake kutumia vyakula vyenye folic acid miezi mitatu hadi sita kabla ya ujauzito wao.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Bima ya Strategies, Dk. Flora Minja (kushoto), akikabidhi mahitaji muhimu ya wazazi kwa Zulpha Abdul, katika wodi ya wazazi ya Hospitali ya Mkoa ya Mwananyamala, mkoani Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya kampuni hiyo kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makada CCM Ubungo waelekezwa kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, kimeelekeza makada wake kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19.

Mwenyekiti CCM wa wilaya hiyo, Lucas Mgonja alisema, Ubungo ina ofisi 90 za serikali za mitaa na vituo 50 vya kutolea chanjo hiyo, na kwamba kila kada kwa nafasi yake inatakiwa kuhimiza.

"Kama chama, tuna wajibu kuhamasisha chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo, hivyo njia mojawapo tunayotumia, ni kuwahimiza makada kwenye ngazi ya serikali za mitaa kufanya kazi hiyo," alisema Mgonja.

Alisema, pamoja na kwamba chanjo hiari, suala la kuhamasisha ni la muhimu, kwa kuwa, kumekuwapo na upotoshaji ambao unaweza kusababisha watu wanaotaka kuchanja wawe na hofu.

"Lakini ninaamini kwamba, uhamasishaji huo unaoambatana na elimu sahihi kutoka kwa wataalam wa afya walio kwenye vitu vya kutolea chanjo, unaweza kusaidia watu kujitokeza kwa wingi kuchanja," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema, chama hicho kina makada wengi na wenye ushawishi mkubwa katika jamii, na kwamba hamasa yao kwenye suala la chanjo inaweza kuwa na mchango mkubwa.

"Elimu ya kuhusu chanjo ni jukumu la wataalamu wa afya, sisi wajibu wetu ni kutoa hamasa kwa wananchi ili wajitokeze kwa wingi kupata elimu hiyo kisha waamue kwa hiari yao kwenda kupata chanjo," alisema.

Alisema, wao kama chama wanaamini kuwa kasi ya utoaji wa elimu ya chanjo inahitajika zaidi, hasa kutokana na idadi ndogo ya watu ambao wamejitokeza kuchanja tangu huduma hiyo ilipoanza kutolewa mwaka jana.

"Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe alishatoa taarifa kwa umma kuwa hadi kufikia Februari 6 mwaka huu, ni watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 waliokuwa wamepata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19," alisema.

Mgonja alisema, kwa takwimu hizo ni wazi ipo haja ya kuongeza kasi ya uhamasishaji ili watu wengi zaidi wachanjwe, na kwamba kwa upande wao CCM Ubungo wanatumia makada kuhamasisha.

Alisema, vyama vya siasa ikiwamo CCM vina mchango mkubwa kwenye suala la chanjo ya UVIKO-19, kwa kuwa vina wanachama ambao ni muhimu wahamasishwe na waelimishwe ili wachanjwe.

# Wadau walilia usawa matumizi ya mitandao

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA kuadhimisha Siku wa Wanawake Duniani, wadau wa haki ya kutumia mitandao nchini wameiomba serikali kushughulikia changamoto zinazotokana na matumizi ya mtandao nchini ili kuongeza idadi ya wanawake wanaotumia huduma hiyo na kuleta usawa.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam, katika semina iliyojadili haki za matumizi ya mitandao nchini iliyoandaliwa na taasisi zinazotetea haki ya kutumia mtandao, Zaina Foundation ya Tanzania ikishirikiana na Paradigm Initiative ya Nigeria.

Akifungua semina hiyo ,Mkurugenzi Mtendaji wa Zaina Foundation, Zaituni Njovu, alisema takwimu zinaonyesha kuna idadi ndogo ya wanawake wanaotumia mitandao ukilinganisha na wanaume.

"Mfano Takwimu za Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), zinaonyesha ni asilimia 17 tu ya wanawake nchini wanatumia mitandao kulinganisha na asilimia 35 ya wanaume, tunaona hapa kuna 'gap' (pengo) kubwa linahitaji kuzibwa ili kuleta usawa, " alisema Zaituni.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazochochea kuwapo kwa pengo hilo ni miundombinu ya upatikanaji wa mtandao pamoja na gharama kuwa juu na kuomba serikali kuifanyia kazi ili wanawake wengi zaidi waweze kuipata haki hiyo.

"Tunapenda kuijulisha serikali kuwa gharama kubwa katika huduma hiyo tofauti na vipato vyao ni sababu ya wanawake kutotumia mitandao, lakini kwa maeneo ya vijijini bado mitandao ni ya shida mpaka ukae eneo fulani ndio upate huduma," alisema Zaituni. Alisema pia kumekuwa na unyanyasaji wa wanawake katika mitandao ya kijamii hali inayowafanya kundi hilo kujiweka pembeni na matumizi hayo, hivyo kuiomba serikali kupitia upya sheria ya mtandao.


"Tunaiomba pia serikali ipitie upya sheria za matumizi ya mitandao ili kuwabana wale wanaotoa lugha za kuwanyanyasa na kuwakosesha kutumia mitandao ya kijamii wenzao ili kila mmoja aweze kuitumia haki yake ya kutumia mtandao, " aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Myhealth Foundation,Dk Harieth Mkaanga, alisema Watanzania wanapaswa kuelewa kuwa ni haki ya kila mmoja wao kupata kutumia mtandao kwa kutoa au kupokea taarifa.

Dk. Mkaanga aliiomba serikali kuliangalia suala la haki ya mtandao kwa kina kwa kuwa kuna unyanyasaji wa wanawake unaoendelea na unasababisha jamii kukosa maarifa mazuri kutoka kwa wanawake.

Naye Furaha Libangu, Mratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka Manispaa ya Kinondoni, alisema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuleta usawa wa matumizi ya mitandao nchini na kuhakikisha kuwa kila mwananchi anaitumia haki hiyo bila bughudha.

"Kwa kuwa sasa tunatambua chanzo cha tatizo letu, tunawakaribisha Zaina Foundation na wadau wengine mje mshirikiane na serikali kwa pamoja tujadili ni kwa namna gani tunaweza kuliweka jambo hili sawa," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mawasiliano ya TTCL, Waziri Kindamba (kulia walioketi) na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Teknolojia ya Huawei Tanzania, Damon Zhang (kushoto walioketi), wakitia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji utakaoziwezesha pande hizo mbili kushirikiana katika kuboresha teknolojia ya mawasiliano nchini. Anayeshuhudia ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (nyuma). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Huawei, TTCL kuboresha teknolojia ya mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mawasiliano ya TTCL na Kampuni ya Teknolojia ya Huawei, wametia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano wa kiutendaji utakaoziwezesha pande hizo kushirikiana katika kuboresha teknolojia ya mawasiliano nchini.

Makubaliano hayo pia yanahusisha uunganishaji wa huduma ya uhakika ya mtandao wa intaneti majumbani (FTTH),upanuzi wa huduma ya intaneti yenye kasi (4G), na upanuzi wa huduma hizo hususani maeneo ya vijijini.

Hati hiyo ya ushirikiano ilisainiwa katika kilele cha Siku ya Biashara kwa Tanzania katika maonyesho ya Biashara ya Dubai Expo 2020 yaliyofanyika, Dubai, Falme za Kiarabu hivi karibuni ambapo Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Akizungumzia makubaliano hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Waziri Kindamba, alisema ushirikiano huo alieleza kuwa makubaliano hayo yanalenga katika kuziwesha pande zote mbili kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kiutendaji hatua ambayo italisaidia shirika hilo kujijengea uwezo wa kiufanisi hususani katika kipindi hiki ambacho Tanzania inapitia mabadiliko ya kidijitali yanayoakisiwa na ongezeko la watu wanaounganishwa kwenye huduma za mawasiliano na mtandao.

"Naweza kusema ushirikiano huu na kampuni ya Huawei Technologies umekuja wakati mwafaka sana, kwani kwa kiasi kikubwa utachangia katika kuifanya nchi yetu kuwa ya kidijitali. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa kila mteja anaunganishwa na huduma za mtandao za haraka na bora." Alisema.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Huawei Tanzania, Damon Zhang alisema kuwa nia ya Kampuni ya Huawei katika kushirikiana na TTCL ni matokeo ya kutambua kuwa miundombinu ni jambo lenye umuhimu zaidi katika maendeleo ya sekta yoyote, hasa sekta ya Mawasiliano," alisema na kuongeza:

"Hatua yetu ya kushirikiana na TTCL ni matokeo ya Huawei kutambua ukweli kwamba miundombinu ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya sekta ya mawasiliano nchini. Tunawahakikishia dhamira yetu ya kuendelea kushirikiana na serikali na mashirika yake ili kuhakikisha Tanzania inaunganishwa kikamilifu."

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Prof. Godius Kahyarara, pamoja na kupongeza hatua hiyo, alisema kuwa ushirikiano kati ya mashirika hayo mawili utaijengea uwezo kampuni ya Mawasiliano ya TTCL katika sekta ya TEHAMA na maeneo mengine.

Utiaji saini wa hati ya makubaliano kati ya Kampuni ya Teknolojia ya Huawei na TTCL ulishuhudiwa pia na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

## LHRC yataja mambo 3 ya usawa kijinsia

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimekuja na mapendekezo matatu, ambayo kinaamini kuwa yanaweza kusaidia kuimarisha na kufanikisha usawa wa kijinsia ipasavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, ndiye aliyetoa mapendekezo hayo jijini Dar es Salaam jana alipotoa tamko la LHRC kwa waandishi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alitaja mojawapo ya mapendekezo hayo kuwa ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia na haki za wanawake, kuimarisha huduma za jamii na kusaidia wanawake wanapopata changamoto za ukatili.

"Tunashauri kutengeneza sheria mahsusi ya ukatili wa kijinsia ili kulinda wanawake na jamii kwa ujumla dhidi ya vitendo vya ukatili, kurekebisha sheria kandamizi zinazoendelea kuathiri wanawake," alisema Henga.

Alitaja pendekezo lingine ni kutofumbia macho vitendo vyovyote vya ukatili na kiutoa taarifa pale wanapoona mtu anafanyiwa ukatili na pia kuachana na mila na desturi zilizopitwa na wakati zinazokandamiza ustawi wa mwanamke.

"Lakini tunapendekeza kuwapa nafasi wanawake kuonyesha uwezo wao ikiwamo kwenye uongozi katika ngazi za maamuzi, lakini pia wanawake wenyewe wajiamini na kuamini kuwa wanaweza," alisema.

Aliwataka wanawake kutumia fursa zilizoko kujiendeleza na kuhakikisha wanapata elimu ya kutosha inayohusiana na masuala yanayowahusu, na kwamba waendelee kuwa chachu ya kukemea mfumo unaowakandamiza.

Alisema, Tanzania inayoamini na kusimamia usawa wa kijinsia inawezekana, na kwamba haki za wanawake ni haki za binadamu, na kwamba vitendo vya unyanyasaji vinavyowabagua ni sawa na kuvunja haki zao za msingi.

Aidha, alisema, pamoja na hayo, tangu mwaka 1997, Tanzania imeshuhudia mabadiliko mbalimbali katika masuala ya uongozi pamoja na mipango madhubuti yenye lengo la kuufikia usawa wa kijinsia.

"Mabadiliko hayo ni pamoja na uteuzi mbalimbali wa wanawake katika nafasi za uongozi ambazo hazikuwahi kushikiliwa na mwanamke kama Waziri wa Ulinzi, Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu na Katibu wa Bunge," alisema.



Ukurasa 12

**KITIMOTO UKRAINE**

**Wanafunzi wanavyohaha kusoma, kuokoa maisha**




Ukurasa 13

Tausi Coffee jina linalotikisa kisiasa, kiuwekezaji




Ukurasa 14

**Aisha Machano - Mwenezi BAWACHA:Tuliko, usajili kielektroniki**

siasa

JUMATANO MACHI 9, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Jicho la wachambuzi kuhusu dira ya CHADEMA yenye Mbowe huru

• Kijo- Bisimba: Dai la Katiba Mpya • Mwakatobe: Uamuzi mgumu waja • Mhadhiri: Serikali imethubutu

**Na Sabato Kasika**

HABARI za kuachiwa huru Mwenyekiti wa CHADEMA , Freeman Mbowe, ndilo jambo linaloendelea 'kutrend' kwenye mitandao.

Tangu mwishoni mwa wiki miongoni mwa taarifa zinazoendelea kuzungumzwa na watu wa kada mbalimbali na kuandikwa katika vyombo vya habari, ni kuachiwa huru Mwenyekiti Mbowe

Kila mmoja anaongea lake kuhusu maendeleo ya chama hicho baada ya mwanasiasa huyo kuwa huru na kwamba huenda chama kikaimarika zaidi kwa haraka, au akawa na kazi kubwa tena ya kurekebisha iwapo kuna mdororo.

Nipashe inazungumza na baadhi ya wachambuzi wa siasa kufahamu kipi ambacho wanakiona kwa chama hicho baada ya Mwenyekiti wa Taifa kuungana na viongozi wenzake, akipotezana nao kwa miezi nane aliyoitumia rumande.

Dk. Hellen Kijo-Bisimba, mwanaharakati na mtetezi wa haki za binadamu, tangu akiwa Mkurugenzi Mtendaji Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), anasema Mbowe kuwa huru ni mwanzo kuendeleza ajenda ya katiba mpya.

"Ninaamini chama kinaweza kuja na nguvu mpya ya kuendeleza ajenda ya kudai katiba mpya, kuandaa mkutano mkuu ili kujadili mambo mbalimbali likiwamo sakata la wabunge wa viti maalumu," anasema Dk. Hellen.

Anasema, ajenda hizo zilikatishwa baada ya Mbowe kukamatwa na kwamba viongozi wa chama hicho waliweka pembeni masuala hayo na kuelekeza nguvu katika kushughulikia kesi ya mwenyekiti wao.

Mwanaharakati huyo anasema, anasikia taarifa za kurudi nchini Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA anayeishi ughaibuni, Tundu Lissu, na kwamba kama zina ukweli, kuna uwezekano wa CHADEMA kuibuka kwa kishindo.

"Ninasema hivyo kwa sababu watu hao wana ushawishi mkubwa kwa umma, lakini cha msingi ni kufanya siasa za kistaarabu kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiagiza ili kujenga nchi kwa pamoja," anasema.

**MAAMUZI MAGUMU**

Mchambuzi wa siasa Gwandumi Mwakatobe anasema, chama hicho kinaweza kufanya maamuzi magumu hasa kwenye suala la wabunge 19 wa viti maalumu ambao wamekuwa ni gumzo kubwa.

"Kimsingi siyo rahisi kutabiri kwani wachambuzi si watabiri bali wanachambua kile ambacho tayari kimetokea, lakini kwa suala la Mbowe kuwa huru ninadhani sasa mkutano mkuu utafanyika," anasema Gwandumi.

Aidha, miongoni mwa ajenda ambazo zimekuwa zikisubiriwa kwa hamu, ni kuhusu wabunge hao, na kwamba hilo ndilo ambalo linamfanya aseme kuwa huenda chama kikafanya uamuzi wa kuwatimua wabunge hao.

"Sisi tunasikiliza watakavyopanga wenyewe, hivyo ni vyema tusubiri kwani hata bunge linasema halina tatizo kuhusu kuwaondoa bungeni wabunge hao bali linasubiri taarifa kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi," anasema.

Gwandumi anafafanua kuwa , hicho ndicho kikubwa anachokiona mbele baada ya Mbowe kuwa huru, na kwamba suala la chama kudai katiba mpya linajulikana kwa maelezo kwamba hilo ni hitaji la Watanzania wote.



Dokta Hellen Kijo-Bisimba, anaamini juhudi za kuomba kuandikwa katiba mpya zitaendelea. **PICHA: MTANDAO**

**MARIDHIANO KWANZA**

Godwin Gonde ni Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia na mchambuzi wa siasa, ambaye anasema hawezi kupima hatima ya chama hicho bali anaangalia uthubutu wa serikali wa kutafuta maridhiano ya kisiasa.

"Katika awamu ya tano, kulikuwa na sintofahamu kwenye siasa za Tanzania hasa kwa vyama vya upinzani, lakini awamu ya sita imekuja na mfumo wa kutafuta maridhiano ambayo kwa kweli ni nzuri na unaofariji," anasema Gonde.

Anasema, anachokiona ni kuendelea kuimarika kwa demokrasia nchini, ambayo anasema miaka ya nyuma ilikumbwa na ukakasi kidogo na kusababisha vyama kushindwa kufanya shughuli zake.

"Viongozi wa chama hicho, wanajua wamejipangaje, hasa kwenye mambo yanayohusu chama chao ikiwamo suala la kudai katiba mpya na sakata la wale wabunge wa viti maalumu, siwezi kuwasemea," anasema.

"Suala si kuangalia kuwa CHADEMA itakuwa ya aina gani baada ya Mbowe kuachiwa huru, bali cha msingi ni uthubutu wa serikali wa kutaka kuimarisha demokrasia kwa kutafuta maridhiano ya kisiasa," anasema mwanazuoni huyo.

Mchambuzi huyo anasema, kama kuna mambo ya msingi ambayo Rais na viongozi wa CHADEMA wameafikiana, naomba yaheshimiwe na hasa suala la kufanya siasa za kistaarabu.

**MBOWE YU HURU**

Machi 4 mwaka huu, mwanasiasa huyo aliachiwa huru ambapo tangu kutiwa mbaroni mwaka jana hadi alipoachiwa huru, kulikuwapo na wito kutoka kwa watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini waliotaka asamehewe.

Kesi yake ilikuwa ni moja ya mambo yaliyoteka karibu maeneo yote ya nchi na kwingineko duniani, huku pia wanadiplomasia wa nchi za magharibi wakifika wakati wote mahakamani kufuatilia mwenendo wa kesi hiyo.

Baada ya kuachiwa huru, mwanasiasa huyo alikutana na Rais Samia Ikulu na kufanya mazungumzo, huku Mbowe akimshukuru Rais kwa kuonyesha kujali na kwamba, msingi mkuu wa kujenga taifa ni kusimamia katika haki na ukweli.

Pamoja na hayo, Mbowe akakaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa walikubaliana kufanya siasa kwa kistaarabu na za kiungwana, na kwamba, yuko tayari kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo.

KITIMOTO UKRAINE

# Wanafunzi wanavyohaha kusoma, kuokoa maisha

**Na Christina Mwakangale**

TANGU Februari 24 mwaka huu, yamkini si shwari tena nchini Ukraine kufuatia mzozo baina yake na Russia. Hivyo ni vyema kuangalia hali halisi inayodaiwa imechochea vitu baina ya ndugu hao.

Kwa kurejea historia za mataifa hayo yanayopambana kwa lugha za wenyeji jina la taifa hilo linalopigwa linatamkwa Ukraina-siyo Yukrein kwa Kiingreza au lilivyozoeleka.

Ukraina ilikuwa sehemu ya Jamhuri za Kisovieti USSR, nchi hizo zina udugu wa asili tangu enzi za muungano .

Kihistoria mji mkuu wa nchi ya Russia iliitwa 'Russ' iliyozaa Urusi au Rossiya kwa lugha za wenyeji.

Mji mkuu wa Byeloruss ambayo leo huitwa Belarus na Ukraina ulikuwa Kiiv, au Kiev ambao leo ni makao makuu ya Ukraina.

Warusi na Waukraina na Wabyeloruss ni wamoja kihistoria, kiutamaduni, kiserikali na hata kijeshi.

Wamekuwa pamoja enzi zote kabla na baada ya vita nyingi vikiwamo vita vya wababe wawili Wakomonist na Mabeberu maarufu vita baridi.

Yukraina ni kipenzi cha Urusi inazo siri nyingi za Urusi, taarifa za kijeshi na silaha, za Rossiya na Byeloruss hivyo ni mambo ya ndani.

Watu hawa ni wamoja na hata lugha zao na madhehebu yao ni ya 'Pravoslavniy au Orthodox.

Baada ya kusambaratika Muungano wa Kisoviet , Byeloruss na Ukraina zilijitangazia uhuru kamili.

Lakini, vita inazuka kwa sababu ya kitendo cha Ukraina kutaka kujiunga na Umoja wa Majeshi ya Kujihami ya Magharibi-NATO.

Ikumbukwe NATO alikuwa hasimu wao mkubwa kwa miaka mingi hasa enzi za vita baridi ikihusisha Urusi na Marekani na hata leo pia ni mahasimu wa miaka mingi.

Hivyo kwa mujibu wa Urusi, nia au tafsiri ya kuikaribisha NATO Ukraina ni hatari ni kitisho kwa uwapo wa Russia yenyewe ambayo ndiye mrithi mkuu wa iliyokuwa Jamhuri za Kisovieti.

**WANAFUNZI UKRAINA**

Baada ya kuangalia kiini cha vita ni wakati wa kutazama hatima ya wanafunzi walioko Ukraina na yapi matazamio na changamoto wanazozipata wakati taifa wanakosomea likiwa vitani.

Tangu miaka ya 1960 wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali duniani wamekuwa wakisaka elimu hasa ya juu ughaibuni.

Hata kwa nchi za Afrika Mashariki, wanafunzi walijielimisha kwenye vyuo vya nchi wanachama vya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakisoma kwenye chuo cha Makerere, Uganda kilichokuwa maarufu miaka hiyo.

Aidha, vyuo vingine maarufu barani Afrika kama Nairobi Kenya kadhalika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho pia wamesoma viongozi kadhaa wa Afrika ni moja ya mifano ya kusaka elimu 'majuu'.



Katibu Mkuu wa NATO Jens Stoltenberg. Alianza kuongoza majeshi hayo mahasimu wa Russia kuanzia 2014 ndiye anayetazamwa kwenye vita hiyo. **PICHA: MTANDAO**

> Sina muda kusema nianze masomo ninachohitaji ni shahada yangu. Labda nimalizie shahada ya pili sehemu nyingine.

Vivyo hivyo wazazi, walezi hawakulaza damu ilipotokea fursa kimasomo nje ya bara la Afrika, kulikopatikana udhamini wa masomo tangu mwanzo hadi kuhitimu shahada kwenye fani tofauti.

Utamaduni huo umejengeka hadi sasa ndiyo maana vita ya Urusi na Ukraina imewanasa wanafunzi walioko kwenye vyuo vyake ambao wameathiriwa na mapambano wakiwamo kutoka barani Afrika.

Wapo Watanzania, Waangola, Wacongo, Waghana, Wanaigeria na raia wa nchi nyingine nyingi, ambao walikuwa nchini humo kusoma elimu ya juu.

Inakadiriwa wanafunzi kutoka Afrika, Asia na Mashariki ya Kati ni takribani 76,000 wanasoma nchini Ukraine, kwa mujibu wa data za nchi hiyo za mwaka 2020.

Pia, robo ya wanafunzi hao hutoka Afrika wengi wao ni raia wa Nigeria, Morocco na Misri huku India ikiwa na wanafunzi wengi zaidi, takribani 20,000.

Wengi wa wanafunzi hao wamefuata ujuzi tofauti nchini Ukraine kama vile kozi ya tiba na afya, uhandisi na biashara.

**KWANINI UKRAINE**

Huenda wapo wanaojiuliza kipi kiliwavutia kusoma Ukraine?

Kwa mujibu wa vyombo vya habari mbalimbali vya kimataifa, Ukraine imekuwa ikipokea wanafunzi kutoka nje kwa miaka mingi tangu zama za Shirikisho la Kisovieti na kwamba nchi nyingi za Kiafrika zilivutiwa kutokana na uwekezaji uliowekwa huko kwenye elimu ya juu.

Hivi karibuni vyuo vya Ukraine vilitumiwa kama lango kuu la 'kutoka' au kupata mchongo kuelekea nchi za Ulaya, aidha fursa za kazi ama ujuzi zaidi wa gharama nafuu ulipatikana ikilinganishwa na vyuo vingine.

Vilevile upatikanaji wa nyaraka za kusafiria visa ni rahisi na wengine hufanikiwa kupata uraia au ukazi wa kudumu kutokea nchini humo.

"Shahada ya Ukraine inatambuliwa na ni ya kiwango chenye hadhi," anasema Patrick Esugunum, anayefanya kazi kwenye taasisi ambayo hutoa mwongozo kwa wanafunzi kutoka Afrika Magharibi wanaohitaji kusoma Ukraine.

Desmond Chinaza Muokwudo, mwanafunzi wa Kinigeria anayeishi jiji la Dnipro Ukraine, anasema alivutiwa na kujiunga na masomo huko kutokana na vigezo vya kujiunga kuwa vya masharti nafuu, rahisi na maisha nafuu ikilinganishwa na miji mingine na vyuo barani Ulaya.

Alijiunga na Chuo cha Kodi na Fedha, miezi mitatu iliyopita huko Ukraine akisema:"Kozi nyingi zinatolewa kwa Kiingereza na aliye na miaka 30 anapata fursa ya kujifunza Kiukraine kabla kusonga mbele na masomo ya uhusiano wa kimataifa.Narudi Nigeria, natamani kumaliza masomo yangu,"

Anasema mwanafunzi huyo akiwa kwenye hosteli nchini Poland baada ya kukimbia vita Ukraine.

**WALIOKIMBIA VITA**

Taarifa zinasema inakadiriwa kuwa zaidi ya wanafunzi 10,000 kutoka Afrika wamefanikiwa kukimbia vita vinavyoendelea Ukraine, na kwenda nchi jirani kwa mujibu wa habari zilizopatikana kutoka vyanzo vya Umoja wa Ulaya (EU).

Pia, kwa mujibu wa video kadhaa mtandaoni, kuna taarifa kwamba wanafunzi wa kigeni wanakumbwa na ubaguzi wa kutopewa kipaumbele cha kuondoka Ukraine na kulazimika kutumia fedha zao binafsi kukodi usafiri hadi nchi jirani.

Serikali ya Ukraine imezindua mpango maalum wa mawasiliano mtandaoni kwa ajili ya wanafunzi wa Kiafrika na Kihindi wanaotaka kukimbia vita, kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba.

**MASOMO KUENDELEA?**

Wanafunzi hao walipohojiwa na vyombo vya habari,wanasema tayari wamewekeza pakubwa katika elimu yao kutoka Ukraine, hivyo bora wasalie barani Ulaya kuhitimisha masomo ya shahada wanazosoma

Jessica Orakpo, ambaye yupo mwaka wa sita akisomea tiba, katika Chuo Kikuu cha Ternopil National Medical, alibakiza miezi minne kuhitimu kabla ya Russia haijaivamia Ukraine kijeshi.

"Nimekwama sasa, siwezi kwenda mbele na elimu kwa sababu chuo changu ndicho kina nyaraka zangu zote kuhusu fani yangu," anasema hayo akiwa njiani kuelekea mji mkuu wa Hungary, Budapest.

"Sina muda kusema nianze masomo ninachohitaji ni shahada yangu. Labda nimalizie shahada ya pili sehemu nyingine."

Nchini Ghana, taasisi za elimu ya juu zimetangaza kwamba baadhi ya wanafunzi waliokimbia Ukraine, watapata fursa ya kuhitimu masomo yao kwenye vyuo vya nchi hizo.

Muokwudo, ambaye sasa anaishi Poland atajaribu kumaliza kozi yake Ulaya iwapo njia zote zitakwama, akisema atabaki hapa aone hali inakwenda namna gani.

**MITANDAO**

# Tausi Coffee jina linalotikisa kisiasa, kiuwekezaji Shinyanga

**Na Gaudensia Mngumi**

- Mama alianza na dagaa, sasa ana kiwanda
- Mtaji wa kilo 5 kahawa leo umezaa tani 250

DIWANI wa Kata ya Ndala mkoani Shinyanga Zamda Shabani maarufu 'Tausi' ni mwanasiasa na mjasiriamali mwanamama anayeishi na kutembelea fikra hizi,'tufanye kila juhudi tubadili maisha yetu.'

Chapa hiyo akilini, ndiyo iliyomtoa Zamda kwenye umaskini, tena akiwa yatima aliyepoteza wazazi utotoni na kumnyanyua kutoka kwenye ufukara wa kipato, fikra,elimu kisha kuingia katika dunia mpya ya mafanikio kijamii, kisiasa na kiuchumi licha ya kwamba alisoma hadi darasa la saba tena akisema ni kwa taabu nyingi.

"Nilisoma Kigoma miaka ya 90 na kumaliza la saba, sikuwa na wazazi nimelelewa na kutunzwa na wajomba nilifika Shinyanga kutafuta maisha na huo ukawa ufunguo wa kuingia kwenye maisha haya." anasema Zamda.

**MBIGIRI ZILIMTOBOA**

Anapozungumza wakati huu dunia ikiadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani, anaweza kufananishwa na mpiganaji ambaye licha ya kushambuliwa mara 99 alinusurika, kunyanyuka na kusonga mbele akiwa mtetezi na msaidizi wa wanawake ili wafikie maendeleo.

Tena ni mwekezaji anayemiliki kiwanda na kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali na pia mwajiri mwenye wafanyakazi wenye ajira rasmi takribani 25.

Anaiambia Nipashe kwenye mahojiano kuwa ni mwanasiasa, diwani wa CCM Kata ya Ndala tangu 2020, akipata ushindi baada ya kuvuka kiunzi cha wanaume 18 waliokuwa wanasaka nafasi hiyo, naye pekee akisimama kama mama.

Anaongeza "Haikuwa rahisi, lakini siasa ninaifahamu imejaa kashfa, figisu, niliitwa mchawi , mfuga nyoka na chatu anayeishi karibu na mto. Mambo mabaya mengi na makubwa yalitajwa kwangu. Lakini, mwishoni nilikubalika leo ninaongoza Ndala , ni diwani."

Anakumbusha kuwa alianza harakati za siasa tangu 2002 akiwa mjumbe wa kamati ya siasa, kata ya Ndala. Hakupoa 2007 akachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Kata ya Ndala, kazi aliyoifanya hadi alipoingia kwenye udiwani.

"Nisema wanawake tunatakiwa kuamua na kujiamini na kufanya kila juhudi ili tufanikiwe hata kama tunaona kuwa tuko mkiani."

Anaongeza kuwa hata kwenye uwekezaji fursa za kiuchumi hakuna aliyezaliwa nazo ni kujitambua , kujituma na kuamua kujikwamua.

**UWEKEZAJI MKONONI**

Zamda anasema kinachomtambulisha kwenye masuala ya uwekezaji ni kiwanda cha kahawa cha 'Tausi Coffee'anachomiliki, kilichopo Ndala mjini Shinyanga. Kinakaanga, kusaga, kufungasha kahawa na kuuza mikoa ya Mwanza,




'Super woman' Zamda Shaban akizungumzia bidhaa ya Tausi Coffee (picha ndogo) inayotangaza juhudi na kazi zake. **PICHA: MWANDISHI WETU**




Mara, Singida,Tabora, Simiyu na wateja wengine ni wa Dodoma.

"Ninachakata tani takribani 200 kwa mwaka. Ni wastani wa tani 15 kwa mwezi. Ninanunua kutoka kwenye kampuni na mashirika wanaoitoa kahawa kwa wakulima huko Bukoba. Nina bidhaa nyingine kama mafuta ya alizeti nachakata karibu tani 250 kwa mwaka," anasema mwanasiasa huyo anayejiamini.

Aidha, ananunua alizeti kutoka kwa wakulima wa Shinyanga, Simiyu na Bariadi na pia anasaga viungo hasa 'mchuzi mix' akinunua viungo kutoka masoko ya Tanga, Dar na Morogoro.

Kadhalika mwanamama huyo, anasaga na kusambaza unga wa lishe wenye virutubisho muhimu kwa watoto ,wazee na wagonjwa mbalimbali.Viwanda hivyo vimeajiri wafanyakazi 27 walio na ajira rasmi ni 15.

**HISTORIA YAKE**

Anasema alianza biashara akiwa na miaka 18 mwishoni mwa miaka ya 90 akiuza dagaa na vitunguu kwenye soko la nguzo nane Shinyanga Mjini. Baadaye akaendelea na biashara ya maandazi , mihogo ya kukaanga mboga na nyanya alizokuwa anatembeza kwenye mabeseni.

**KILO 5 HADI TANI 5**

"Nilikuwa pia nauza mboga za jumla nikizitoa vijijini kwa kutumia baiskeli. Yote tisa, nikaona bado sijafanikiwa nikabadilisha kuanzia mwaka 2002 nikaingia kwenye kahawa. Nilianza na kilo tano.Nakaanga kwenye karai nafungasha na kuuza ilikuwa kazi ngumu. Nilikuwa napata hasara sikuwa na utaalamu,ujuzi wala mbinu za kibiashara. "

"Nilifahamika duniani kupitia program ya Kampuni ya Bia (TBL) ya kuendeleza wajasiriamali. Ilituunganisha na Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO). Walinitembelea na kuniwezesha kiteknolojia kwa kunipa mashine inayotumia mkaa na umeme kukaanga kahawa".

Aidha, baadaye kahawa iliadimika mno akaachana nayo, akajitosa kwenye bodaboda kazi aliyoifanya kwa miaka nane mfululizo, hata hivyo alirejea tena kwenye kahawa na kuanza uzalishaji kwa tija zaidi.

"Nimeongeza bidhaa nyingine kama mafuta, viungo 'mchuzi mix' na ungalishe." Anaeleza.

> "Nilifahamika duniani kupitia programu ya Kampuni ya Bia (TBL) ya kuendeleza wajasiriamali. Ili tuunganishe na Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO).

**VIPI MITAJI?**

Biashara nyingi zinahitaji mtaji mkubwa, Zamda aliupata wapi? Anasema kukopa hakukwepeki iwapo unataka kuwa na uwekezaji wenye tija licha ya ukweli kuwa mkopo ni harusi na kulipa ni matanga.

"Ni lazima uwe na malengo. Unakwenda kukopa kuanzisha au kuendeleza biashara? Usikope kuanzisha biashara hakikisha kuwa unayo ili uiendeleze kama huna utahangaika. Mimi ninakopa na kurejesha na ndiyo uwekezaji"

Anachotamani sasa ili awe wa viwango zaidi ni mashine za kisasa za kuchakata, kukaanga, kupooza, kusaga na kufungasha kiwango kikubwa cha kahawa.

**KUSAIDIA WANAWAKE**

Diwani huyo, anasema pamoja na siasa na uwekezaji anafanya juhudi kuwainua wanawake wengine, akianzisha na kusimamia vikundi kadhaa vya wanawake akisema:"Nina malengo na matamanio ya kuona kinamama wanajitegemea wakisimama wenyewe ili kuachana na utegemezi."

Zamda anaongeza kuwa changamoto inakuwa kubwa kwa vile wanawake wakipata ujauzito wenza wao wanawakimbia na kuwatelekeza na watoto.

"Nina vikundi kadhaa vya wanawake kama wakulima wa mboga za mchicha, matembele, kuna kikundi cha kuzalisha sabuni na mafuta ya kupaka, kundi la kinamama wanaolima viazi lishe na kutengeneza unga wa lishe pia wapo wafuga kuku,"anasema.

Anaongeza kuwa anashirikiana na wanawake zaidi ya 30, akiwaelekeza masuala ya mikopo ya halmashauri kwa kinamama, vijana na wenye ulemavu na njia bora za kunufaika.

Aidha, anawasaidia kuzalisha kwa tija na ubora, kupata masoko ya bidhaa zao wakati mwingine kwa kutumia mitandao ya intaneti, kujitangaza kupitia fursa za mikusanyiko kama siku ya wanawake duniani na ziara za viongozi mbalimbali akilenga kuwainua na kupunguza umaskini.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Aisha - Mwenezi BAWACHA: Tuliko, usajili kielektroniki

• Kapu moja lenye siasa, uchumi, elimu



Wanachama wa BAWACHA katika harakati za kisiasa na kijamii. **PICHA ZOTE: BAWACHA**

**Na Beatrice Philemon**

ILI wanawake wanufaike na asilimia 10 ya mikopo inayotolewa na halmashauri kwa kinamama,vijana na wenye ulemavu, ni vizuri idara inayosimamia utoaji wa mikopo hiyo kwenye halmashauri isimamie yenyewe badala ya wanawake kupeleka maombi kwa Ofisa Maendeleo Kata, ili ayapeleke kwenye halmashauri.

"Ni kwa sababu wanawake wengi wanalalamika kukosa mikopo wakidhani sababu ni baadhi ya maofisa maendeleo kata kutofikisha maombi yao kwenye halmashauri badala yake yanabakia kwenye mafaili ya maofisa hao," ni maelezo ya Katibu Mwenezi, Baraza la Wanawake Taifa la CHADEMA (BAWACHA) Aisha Machano.

Ni katika mazungumzo na Nipashe wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, akisema serikali isimamie na kuhakikisha asilimia 10 inayotokana na mapato ya halmashauri inawafikia walengwa na kuleta tija.

Analalama kuwa wawawake wengi hawajafikiwa na fedha hizo na kwamba ni muhimu kuangalia mianya inayozipoteza.

Anadai pia kuwa kuna kukwekwa pembeni kwa baadhi ya mipango ya biashara inayowasilishwa kwa maofisa maendeleo ya kata na kuomba eneo hilo litazamwe upya.

Akizungumzia BAWACHA, ilivyowawezesha kinamama kiuchumi anasema ushirikishwaji wa wanawake ndani ya BAWACHA, unahusisha kutumia vikao, fursa zinazokuja ndani ya chama mfano semina, mafunzo juu ya uwezeshaji kiuchumi, kutambua biashara na fursa za kiuchumi na uwekezaji.

Aidha, wanatumia wadau mbalimbali kuomba msaada wa mambo wanayohitaji ili kumwezesha mwanamke kwa mfano fedha au vifaa, lakini hadi sasa hawajafanikiwa kupata vitu hivyo kutokana na sababu mbalimbali.

> Kwa mfano, tulitaka kuzunguka nchi nzima kutoa elimu ya mwanamke na uchumi, usimamizi na umiliki wa ardhi, matumizi bora ya ardhi lakini tulishindwa kwa sababu baraza halina fedha wala usafiri.



Aisha Machano Katibu Mwenezi wa BAWACHA

Baraza la Wanawake lina wanachama zaidi ya 3,000,000 wenye ujuzi wa aina mbalimbali ukiwemo ujasiriamali, biashara ndogo ndogo na utengenezaji wa vifaa vya mikono vya aina nyingi.

Kadhalika, BAWACHA inafundisha wanachama ujasiriamali kama namna ya kutengeneza sabuni za maji, za vipande, usindikaji bidhaa na uzalishaji kwa tija, anasema Aisha.

"Kwa mfano peke yangu nimefundisha wanawake zaidi ya 150 katika majimbo mawili ya wilaya ya Temeke, Kigamboni na Mbagala jinsi ya kutengeneza sabuni za aina mbalimbali ili wanawake washiriki katika masuala ya kiuchumi,'" anasema Aisha.

Anaongeza kuwa kama viongozi wangefurahi, iwapo wadau wangekuja kuwawezesha ili kuwasimamia wanawake kusimama kiuchumi na kisiasa kwa sababu mama akifanya biashara anakuwa hasumbuliwi kwenye siasa.

"Wadau wanaopenda kusaidia BAWACHA tunawakaribisha ili tuweze kuinua wanawake kujikwamua kiuchumi, wasaidie kwa kutoa fedha au vifaa kulingana na mahitaji ya wanachama ili tuwaendeleze kiuchumi," anasema Katibu Mwenezi huyo.

Mdau anaweza kutoa vifaa kwa sababu kuna wanachama wengine wanapenda kupewa au kuwezeshwa vifaa au vitendea kazi badala ya fedha ili wafanye biashara, anasema.

Halikadhalika ndani ya BAWACHA, kuna wajasiriamali wengi wanaopenda kufanya biashara, lakini changamoto kubwa ni namna ya kupata mitaji na kufanya uwekezaji huo, anaeleza Aisha.

Anasema katika utekelezaji wa shughuli zao, wanaongozwa na sera ya chama ya wanawake, akitaja baadhi ya vifungu wanavyotumia kuwa ni mwanamke na uchumi wa soko jamii, siasa za ndani, mwanamke na elimu ya sayansi na teknolojia, ushiriki wa mwanamke katika jamii, huduma za afya kwa mwanamke, usimamizi na umiliki ardhi kwa wanawake.

"Mbali na hilo, suala la kuwezesha mwanamama kiuchumi pamoja na wanawake kushirikishwa katika uchumi, lipo katika kipengele namba tatu cha Sera ya CHADEMA ya Wanawake, kinachosema Mwanamke na Uchumi wa Soko.

"Kwa sababu hii inamfanya atambue ushiriki wake katika sekta binafsi, kuzitambua fursa za kifedha na ushindani wa kiuchumi," anasema Katibu Mwenezi.

**MIPANGO NA SERA**

Aisha , anasema Sera yao ni ya 2019 ndiyo inayowaongoza lakini tangu ilipoandaliwa na kuanza kutumiwa haijaleta mafanikio katika chama na baraza kwa ujumla kwa sababu waliunda sera hiyo kwa kila mbunge au diwani atakayeshinda katika uchaguzi 2020.

Anasema, kila mmoja aende aifanyie kazi katika eneo lake, lakini hawakupata wawakilishi katika uchaguzi huo ndiyo maana bado haijaleta mafanikio katika chama. Mama huyo anasemaa hivi sasa wana mbunge mmoja wa kuchaguliwa kutoka mkoani Rukwa na wana madiwani zaidi ya 80 nchi nzima.

Anataja changamoto wanazokumbana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao kuwa ni kukosa kipato, vyombo vya usafiri na uelewa mdogo wa wanachama wanaowasimamia kazi wanazozifanya kama BAWACHA.

"Kwa mfano, tulitaka kuzunguka nchi nzima kutoa elimu ya mwanamke na uchumi, usimamizi na umiliki wa ardhi, matumizi bora ya ardhi lakini tulishindwa kwa sababu baraza halina fedha wala usafiri," anasema Aisha.

**MAFUNZO YA UONGOZI**

Katika kuadhimisha siku ya mwanamke duniani, baraza hilo linajivunia kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake zaidi ya 100, kati ya hao, wengine wamekuwa wabunge, mafunzo yalitolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali ya Hans Seed Foundation na Centre for Good Governance.

Anasema wanawake waliofanikiwa baada ya mafunzo ni wengi, naye ni mmojawapo wa wanufaika wa mafunzo ya Hans seed Foundation na kwamba mbali na hilo, kuna wabunge ambao chama kimewaondoa kwenye uanachama pia ni wanufaika wa mafunzo hayo.

Aidha, Aisha anabainisha kuwa katika utekelezaji wa majukumu yake, mara nyingi BAWACHA inashirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali NGOs kama vile Tanzania Gender Networking Programme (TGNP) na ULINGO kwenye masuala mbalimbali ya usawa wa kijinsia na ushiriki kwenye uongozi.

**MIPANGO IJAYO**

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, BAWACHA imepanga kusajili wanawake nchi nzima kwa kutumia mfumo wa kidigitali ili kuwafikia na kuwapatia kadi za kielektroniki.

"Lengo kuu ni kupata wanachama wengi wanawake kwa sababu wao ndiyo wanaopiga kura na ndiyo wanafanya maamuzi.

Pia kuhakikisha chama kinafanikiwa kwenye kudai na kupata Tume Huru ya uchaguzi ili kuwa na uchaguzi unaokubalika na wa huru na haki,".





# Wanawake watakiwa kufanya kazi kwa bidii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma wameshauriwa kufanya kazi kwa bidii na mshikamano ili kuhakikisha jiji linasonga mbele katika nyanja zote za maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa na Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Sekunda Kasese, katika mahojiano maalum na waandishi wa habari ofisini kwake.

"Napenda kutumia nafasi hii kuwashauri wanawake katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kufanya kazi kwa bidii, weledi, maarifa na mshikamano ili kuhakikisha jiji letu linasonga mbele katika nyanja zote za maendeleo," alisema Kasese.

Kuhusu kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2022 isemayo "Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu; Tujitokeze Kuhesabiwa", alisema kuwa ni muhimu katika kushirikisha jinsia zote katika mipango ya maendeleo kuanzia ngazi ya jamii na taifa kwa ujumla.

"Wanawake ni kundi kubwa sana katika jamii na wao wakishirikishwa katika mipango ya maendeleo, wanaweza na wanafanya vizuri, hivyo wakijitokeza kuhesabiwa kwa sababu ni sehemu kubwa ya jamii yetu, wataiwezesha serikali kufikia malengo yake," alisema Kasese.

Kuhusu mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na TASAF, alisema unafanya vizuri.

"Mpango wa kunusuru kaya maskini unafanya vizuri na unaendelea kufanya vizuri katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuinua hali ya umaskini wa jamii. Kundi kubwa la walengwa walio katika mpango wa kunusuru kaya maskini ni wanawake. Katika Jiji la Dodoma tuna wanufaika 26,289, kati ya hao 16,101 ni wanawake walio katika rika mbalimbali na 10,188 ni wanaume. Wengi wanaopokea ruzuku ni wanawake.

"Tunajua mwanamke akipokea ruzuku ni fedha inayomsaidia yeye pamoja na kaya kwa ujumla sababu anapochukua fedha hiyo haipeleki katika mambo mengine yasiyofaa mfano ulevi wa kupindukia. Fedha anayopata anaipeleka kwenye biashara ndogondogo na shughuli nyingine za uzalishaji mali ili kuongeza kipato cha kaya," alisema.

# Wanaume wanaosindikiza wenza wao kliniki wazidi kuongezeka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IDADI ya wanaume wanaowasindikiza wenza wao kliniki wakati wa ujauzito na hata baada ya kujifungua, imeongezeka katika Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma hali inayoashiria wameanza kufahamu umuhimu wake.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya Chamwino, Bernadetha Petro, wakati wa mkutano wa kujadili Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ulioandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Women Wake Up (WOWAP) na kushirikisha kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ngazi ya halmashauri.

Petro alisema wanaume wanaowasindikiza wenza wao kwenda kliniki wameongezeka katika wilaya hiyo hali inayoonyesha kinababa wengi sasa wanajua umuhimu wa kuwasindikiza wake zao kliniki wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua.

Alisema lengo la serikali ni kufika asilimia 45, lakini halmashauri imejiwekea malengo ya asilimia 60.

Ofisa huyo alisema wenza kwenda kliniki, hufanya kinamama kuwa na furaha na kufurahia ujauzito ikiwamo kuona wanathaminiwa wao na watoto walioko tumboni, hivyo kuongeza furaha kwenye familia.

Hata hivyo, alisema bado wanatoa elimu ili kupunguza mtazamo hasi uliojengeka muda mrefu wa malezi kuachiwa mama peke yake.

"Kinababa nao wanahusika kwenye malezi kuanzia ngazi ya chini na tunaendelea kuelimisha wananchi juu ya uhusiano mzuri kwenye malezi," alisema Petro.

Pia alisema bado kuna changamoto kubwa kwa wazazi kushindwa kufuatilia watoto wao, hivyo kuwataka kuweka jitihada za kuhakikisha wanasimamia malezi ya watoto. Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, Wakuru Nyaratha, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikiwezesha vikundi vya wanawake ili wakijite kwenye biashara na shughuli za uzalishaji.

Alisema baadhi ya vikundi vilipewa ng'ombe ambapo pia maziwa yamekuwa yakitumika kama lishe kwa watoto na kukuza uchumi wa kaya kwa fedha zitakazopatikana.

Mratibu wa WOWAP, Nasra Suleiman, alisema wajumbe wa Kamati ya MTAKUWWA wanatakiwa kufuatilia kwenye ngazi za jamii kama sehemu ya utekelezaji wa mpango huo.




Wafanyakazi wanawake wa Vodacom Tanzania Mkoa wa Dodoma, (kutoka kulia) Ester Lebasi na Suzana Mwaipopo, wakiwafurahia watoto mapacha waliozaliwa kwenye wodi ya wazazi ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, wakati walipoenda na wenzao kutoa zawadi hospitalini hapo jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Dunia. Kushoto ni mama mzazi wa mapacha hao, Neema Elia. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# H'shauri yazindua taarifa anwani makazi, postikodi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma imezindua ukusanyaji wa taarifa za anwani za makazi na postikodi utakaoendeshwa kwa muda wa siku 30.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika ukumbi wa ofisi ya kata ya Kongwa, huku ukihudhuriwa kwa wingi na wananchi waliojitokeza kupata elimu kuhusiana na umuhimu wa anwani ya makazi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa, Omary Nkullo, alisema anwani za makazi na postikodi ni suala kubwa kitaifa, hivyo kila mmoja anapaswa kuelewa umuhimu wake ili lilete tija kwa nchi.

Nkullo alisema anwani za makazi zitamsaidia kila Mtanzania kuwa na anwani yake itakayomtambulisha yeye na biashara zake kiurahisi katika eneo husika, hivyo ni vema kila mmoja akapata anwani yake.

"Suala hili litawarahisishia watu wa vizazi na vifo, huduma za dharura kama magari ya wagonjwa na zima moto,makampuni ya Simu na posta kufanya kazi kiurahisi," alisema Nkullo.

Naye Mratibu wa Mpango huo Wilaya ya Kongwa, Yoram Salum, alisema ukusanyaji wa anwani za makazi uko kwenye Sera ya Taifa ya Posta na ilani ya Chama Cha Mapinduzi lengo likiwa ni kuweka mfumo wa kuwafikia wananchi kiurahisi.

Salum alisema anwani hizo zitaonyesha namba ya nyumba, jina la barabara inayohudumia nyumba husika na Postikodi yaani namba ya kanda, mkoa, wilaya na kata inakopatikana nyumba husika, hivyo ni rahisi mtu kusaidiwa endapo atapata tatizo.

"Hili suala ni la muhimu sana kwa jamii, hivyo wananchi tunapaswa kujitokeza kwa wingi kupata anwani za makazi," alisema Salum.

Diwani wa Kongwa, White Zuberi, kwa niaba ya wananchi, aliomba serikali kuajiri vijana ambao hawana ajira ili kupata pesa za kujikimu ikiwamo kuongeza kipato chao na kujiinua kiuchumi.

"Vijana wetu wamesoma lakini hawana ajira kwa hiyo zikitokea ajira za muda mfupi kama hizi, tunaomba wapewe kipaumbele ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi," alisema Zuberi.

Alisema hizi ni ajira za muda lakini zinamanufaa kwa vijana waliohitimu masomo yao kujiongezea kipato kutokana na fedha ambazo watalipwa wakati wa zoezi hilo likiendelea kufanyika.



# Nyumba zilizopatiwa chanjo ya polio kuwekewa alama

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKATI utoaji chanjo ya ugonjwa wa polio kwa watoto wenye chini ya miaka mitano, ukatarajiwa kuanza Machi 21, mwaka huu, mkoani Mbeya, Mratibu wa Chanjo Mkoa, Danford Barnabas, amesema umeandaliwa utaratibu maalum wa kuweka alama za tiki katika nyumba ambazo zitakazopata chanjo hizo ili iwe rahisi kubaini ambazo hazijafikiwa.

sambamba na hilo, pia mtoto atakayechanjwa chanjo hiyo atawekewa alama kwenye kidole chake ikiwa ni uthibitisho wa kupata chanjo ya polio.

Barnabas alisema wamepanga kufanya hivyo ili kuhakikisha watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano mkoani Mbeya wanapata chanjo ya polio.

Alisema hadi sasa mkoa wa Mbeya unaendelea na jitihada za kuhakikisha ugonjwa wa polio ambao tayari umeripotiwa nchi jirani ya Malawi wanakabiliana nao kwa kutoa elimu kwa wananchi kutunza mazingira na kuzingatia usafi wa chakula kuanzia maandalizi hadi wakati wa kula.

"Sambamba na kujipanga kutoa chanjo ya polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano nyumba kwa nyumba, pia tutawawekea alama za vidole ikiwa ni uthibitisho kuchanjwa. Tunafanya hivyo ili kuwakinga watoto wetu dhidi ya ugonjwa huo hatari ambao hauna dawa ukishaingia kwenye mwili wa binadamu," alisema.

Barnabas aliwaomba viongozi wa kuanzia vitongoji hadi kata kuendelea kuhamasisha wazazi na walezi kuwapeleka kwenye vituo vya afya watoto wao ili wapatiwe chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Mmoja wa wakazi wa Jiji la Mbeya, Tumaini Richard, alistushwa na taarifa za uwapo wa ugonjwa huo katika nchi jirani ya Malawi na kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka kujikinga.

Alisema kwa kutambua athari za maambukizi ya polio. yuko tayari kumpeleka katika kituo cha afya mtoto wake mwenye umri wa miaka mitatu akachanjwe.

Mkazi huyo aliwaomba kinamama kutowaficha watoto ndani kwa sababu mbalimbali zikiwamo imani potofu badala yake wajitokeze kwa wingi kuwapeleka watoto kupata chanjo hiyo muhimu ambayo itawasaidia kukabiliana na maambukizi ya virusi vya polio.



Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Mbeya, Danford Barnabas, akiwafundisha waandishi wa habari kuhusu namna sahihi ya unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya milipuko, wakati wa mafunzo ya chanjo ya ugonjwa wa UVIKO-19, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wataka nguvu kutangaza vivutio vya utalii Nyanda za Juu Kusini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa utalii na ukarimu mkoani Mbeya wameiomba serikali kuweka mazingira rafiki ambayo yataruhusu vivutio vya utalii vilivyoko mikoa ya Nyanda za Juu Kusini vinatangazwa kwa nguvu zote.

Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini umebarikiwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali lakini havijatangazwa ipasavyo na kusababisha idadi ya watalii wanaotembea kuwa wachache kulinganisha na ukanda wa kaskazini.

Miongoni mwa wadau walitoa mapendekezo hayo ni mwanahabari Felix Mwakyembe ambaye alisema kuna haja kwa wadau na serikali kuandaa mpango kabambe ambao utasaidia kutangaza utalii wa Nyanda za Juu Kusini ili kuvutia watalii na kukuza uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja.

Alisema baada ya kupatiwa mafunzo na Chuo cha Taifa cha Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii wamejifunza masuala mbalimbali kama vile ukarimu wa wateja, afya na usalama wa hoteli mambo ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa kuvutia watalii.

"Ukanda wetu wa Nyanda za Juu Kusini una vivutio vingi sana kulinganisha na kanda nyingine lakini tulichofeli sisi ni kuchelewa kuvitangaza. Wenzatu wa kaskazini tangu uhuru walianza kuvitangaza wakati sisi miaka ya 2000. Kuna tofauti kubwa sasa ni wakati wa kushikamana na kutangaza utalii wetu tusahihishe makosa yetu tusonge mbele," alisema Mwakyembe.

Mwakyembe alikiomba Chuo cha Taifa cha Utalii kuendelea na utoaji wa mafunzo ya utalii na ukarimu katika maeneo mbalimbali nchini ili kusaidia wadau wanahusika katika sekta hiyo wakiwamo mama ntilie, wamiliki wa hoteli, waongoza watalii, wapiga picha, madereva na wahudumu wa afya kujifunza namna bora ya kumuhudumia mteja au mtalii.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia kuongeza idadi kubwa ya watalii kwa sababu watashawishika na huduma bora zinazotolewa kuliko ilivyo sasa ambapo kukosekana kwa ukarimu katika sekta ya utalii mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kumechangia pia idadi ya watalii kuwa ndogo.

Mratibu wa mafunzo ya kukabiliana na Ugonjwa wa UVIKO - 19 katika sekta ya utalii na ukarimu kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Naiman Mbise, alisema serikali kupitia fedha za UVIKO - 19 iliwapatia kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya kutoa mafunzo wa wadau mbalimbali wa sekta ya utalii kwa mikoa minane nchini.

Alisema mafunzo hayo yalihusisha watu wa kada mbalimbali na kwa mkoa wa Mbeya, wananchi 131 walihitimu mafunzo na kupatiwa vyeti na Chuo cha Taifa cha Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Dk. Mbise alibainisha kuwa mafunzo hayo pia yalilenga kuwafundisha mbinu za kuinua vipato vyao kupitia sekta ya utalii kwa kuhakikisha wanakuwa wabunifu.

Akifunga mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema sekta ya utalii imekuwa ikichangia kiasi kikubwa pato la taifa na kwamba uwepo wa mafunzo unasaidia kuchagiza ukusanyaji mkubwa wa fedha zitokanazo na utalii hapa nchini.

Dk. Chuachua alisema mkoa wa Mbeya umebarikiwa kuwa na vivutio mbalimbali vya utalii hivyo aliwakaribisha wawekezaji mkoani humo kujenga hoteli na miundombinu mingine ili kuvutia utalii.

# RC ataka mkazo elimu afya vijijini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KATIKA kuhamasisha wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanaendelea kuhamasika kujiunga na CHF iliyoboreshwa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesema elimu kwa waishio vijijini bado inahitajika kwa sababu mwamko bado ni mdogo.

Homera alisema jana kuwa halmashauri na wilaya zote za mkoa wa Mbeya zinatakiwa kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa ili kufikia lengo.

Pamoja na jitihada hizo, alisema mwamko wa waishio vijijini kujiunga na mfuko huo bado ni mdogo na kuwaomba wataalamu wa afya kuyafikia maeneo hayo.

Alifafanua kuwa kwa mwaka 2021/22 Halmashauri ya Busokelo inaendelea na uhamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa na hadi Januari, mwaka huu, kaya kaya 1,879 kati ya kaya 24,187 ziliandikishwa.

"Wilaya Chunya kaya 3, 743 kati ya 33,573 zenye wanachama 18,102 sawa na asilimia 11.4 huku Kyela ikifikia wastani wa asilimia 5.9 ya lengo kwa kuandikisha kaya 3,180 lakini inaendelea kuhamasisha kupitia mikutano ya hadhara kwa kuwatumia maofisa nane kuwatembelea wananchi," alisema Homera.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema imeandikisha kaya 4,225 zenye wanafamilia 15,898 kazi hiyo likihusisha vijiji vyote 152 kuhamasisha kujiunga na CHF iliyoboreshwa.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Benson Sanga, alisema licha ya kuwahamasisha wananchi kujiunga na CHF iliyoboreshwa, wanaendelea kuwahimiza kuchangia shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Alisema katika kuhakikisha utekelezaji wa wananchi kushiriki ujenzi wa vituo vya afya kwa Wilaya ya Kyela walitoa nguvu kazi ya usombaji matofali, uchimbaji msingi, kumwaga zege la jamvi na lenta, kusogeza mawe na mchanga ambapo nguvu kazi hiyo inathamani ya Sh. milioni 12.





## Wajasiriamali wakumbukwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imetenga Sh. 960,000,000 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali na wafugaji wa nyuki hasa wanawake na Vijana.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akifafanua mgawo wa fedha za ahuweni ya UVIKO-19 na jinsi zitakavyotumika katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema mikakati ya Serikali ya Zanzibar ni kuyawezesha makundi yote ili yashiriki kikamilifu katika kazi za ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi.

Alifahamisha kwa muda mrefu wafugaji wa nyuki waliachwa nyuma na hakuna aliyewashughulikia katika harakati zao za kujikwamua kiuchumi.

"Kwa mara ya kwanza Serikali ya Zanzibar imetenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wafugaji wa nyuki kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema.

Naye Waziri wa Kilimo Umwagiliaji na Ufugaji, Dk. Soud Nahoda alisema zaidi ya wafugaji nyuki 69 wametambuliwa na kusajiliwa ambao wamekuwa wakipata baadhi ya misaada mbalimbali na mbinu za ufugaji wa nyuki wa kisasa.

Alisema amefurahishwa na juhudi za serikali hiyo kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wafugaji wa nyuki.

**Naye Waziri wa Kilimo Umwagiliaji na Ufugaji, Dk. Soud Nahoda alisema zaidi ya wafugaji nyuki 69 wametambuliwa na kusajiliwa ambao wamekuwa wakipata baadhi ya misaada mbalimbali na mbinu za ufugaji wa nyuki wa kisasa.**

# Wananchi wahimizwa kulinda miundombinu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kulinda miundombinu inayojengwa na serikali ili kuleta tija kwa maendeleo ya Watanzania.

Hayo yalielezwa jana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla wakati akizindua mnara wa mawasiliano ya 4 G katika kijiji cha Kizimkazi Mkunguni Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuwa serikali imedhamiria kusogeza huduma za mawasiliano karibu na makazi ya wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa maendeleo.

Alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Mapinduzi ya Zanzibar zimejipanga kuweka fedha maalum zitakazotumika kwa ajili ya kuwasogezea huduma za kijamii wananchi wake.

Aidha Hemed alisema azma ya serikali zote mbili ni kuhakikisha kuwa viongozi wanasimamia vyema fedha za serikali hatua ambayo inarejesha nidhamu kwa watumishi na kuwajibika katika majukumu yao kwa maslahi ya taifa.

Alieleza kuwa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania TTCL kufikisha huduma katika maeneo mbalimbali nchini ni katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na kueleza kuwa jambo hilo ni la msingi kwa Watanzania wote.

Sambamba na hayo Hemed aliwataka wananchi kutumia vyema minara hiyo ili kuongeza kasi za kimaendeleo na kuwataka kuzalisha fursa mbalimbali za ajira zinazopatikana kupitia mitandao.

Alieleza kuwa serikali itaendelea kusogeza huduma za kijamii karibu na maeneo ya wananchi ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa huduma muhimu ikiwamo huduma za simu. Kwa upande wake Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alisema kuwa wizara itahakikisha minara hiyo inabaki salama na kuwataka wananchi kutoa taarifa kwa yeyote atakayebainika kuharibu miundombinu hiyo.

Waziri Rahma alitumia fursa hiyo kukemea tabia ya baadhi ya wasiopenda maendeleo kutumia njia ya simu kutapeli wananchi na kuwataka wananchi kutoa taarifa sehemu husika ili kuwadhibiti wahalifu hao.

Hali kadhalika, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nauye, alisema Wizara kupitia Mfumo wa Mawasiliano itaendelea na usambazaji wa minara ambapo minara zaidi ya hamsini itajengwa Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mawasiliano Tanzania TTCL, Waziri Ndimba alieleza kuwa ujenzi wa mnara huo ni katika mpango wa TTCL kufikisha huduma za mawasiliano mjini na vijijini.

Aidha, alisema uwepo wa minara ya mawasiliano unarahisisha kukua kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.



Mkuu wa TEHAMA Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano Zanzibar, Fatma Muhamed Ali (mwenye kipaza sauti), akitoa maelezo kwa Waziri wa Mawasiliano Zanzibar, Rahma Kassim Ali (kushoto kwake) na Waziri wa Habari, Ma-wasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (katikati), walipotembelea kituo cha mawasiliano cha dharura, Kiembe Samaki, mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kituo cha mawasiliano dharura mkombozi majanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema iwapo kituo cha mawasiliano ya dharura kitafanya kazi kama ilivyo kusudiwa kitaondosha changamoto mbalimbali hasa za mawasiliano kwa waathirika wa majanga.

Alisema watu wengi wanapopata majanga wanakosa mawasiliano ya haraka jambo ambalo limekuwa kero kwa wahusika na kujuwa nini wafanye lakini kituo hicho kimesha kamilisha kiu ya wale wanaofikwa na majanga.

Alisema hayo juzi wakati akikabidhi kituo hicho kwa Waziri wa ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, Kiembe Samaki, Mjini Unguja.

Alisema kituo hicho ni miongoni mwa mradi wa serikali ya Tanzania kuwapa serikali ya Zanzibar kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote Tanzania.

Alifahamisha kuwa kituo hicho kazi yake kubwa ni kupokea taarifa kwa wahanga mbalimbali hasa wavuvi, wagonjwa kama wajawazito, wanaopata majanga ya moto na muhusika kupiga simu namba 190 ambayo bila ya malipo.

Alisema wananchi wasiwe na wasiwasi juu ya kituo hicho kufanyakazi zake na kitafanya kazi muda wote wa saa 24 ili kutatua changamoto za wananchi wa Zanzibar.

Alifahamisha kuwa licha ya kuwapo kwa kituo hicho lakini lazima wafanyakazi wa kituo hicho wafanye kazi kwa kujitolea na uadilifu kinyume na hapo, kituo kitakuwa hakina maana yoyote.

Alisema lazima wizara kuweka mikakati imara ya kufanya ziara za mara kwa mara ili kuona namna utendaji wa kituo hicho unavyoendelea na endapo wakibaini wafanya kazi hawako sawa wawachukulie hatua za kinidhamu. Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alisema kituo hicho kitafanya kazi kama ilivyokusudiwa ili kuwanufaisha wananchi wote wa Zanzibar.

Alisema wao kama wizara hawatokuwa tayari kuona wafanyakazi wa kituo hicho wanafanya kazi kwa mazoea kwa vile lengo lake ni kutoa huduma kwa Wazanzibar wote mijini na vijijini.

Alisema iwapo wahusika watakitumia kituo hicho ipasavyo itakuwa fursa kwa kutatua changamoto za majanga na kufanya wafanyakazi kuwa makini wakati wa kazi zao.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Justina Mashiba, alisema lengo la kituo hicho ni kutowa taarifa kwa wahusika wa majanga ili kupata huduma za usaidizi.

Alisema uamuzi wa kuwapo kwa kituo hicho ni miongoni mwa miradi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Alifahamisha kuwa hivi sasa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Habari na Teknolojia inaushirikiano mzuri na Zanzibar na kwa sasa kuna baadhi ya vituo vya TEHAMA kumi vimejengwa kati ya hivyo sita vipo Unguja na vinne vipo Pemba.

Mnara huo umegharimu jumla ya Sh. milioni 200 ambapo kupitia mfuko wa mawasiliano nchini, wamejipanga kufikisha huduma za mawasiliano katika vijiji vipatavyo 382.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEILA SAID MILANZI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0591-0020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya secondari ya RUANDA mwaka 2018 Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: SO/RB/4668/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



AIKANDE ZAKAYO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye No. S0212-0001 kilichotolewa na MACHAME SECONDAY SCHOOL mwaka 1997 yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/95167/2022.

## KUPOTEA KWA VYETI



AALLY KHALEF NASSORO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2537/0149 kilichotolewa na Ilala Sekondari mwaka 2016. Cheti cha Diploma namba 0101656 kilichotolewa na Kampala International University mwaka 2020. Transcript iliyotolewa na NACTE – DAR mwaka 2020. Leseni ya Diploma namba RPR11500 iliyotolewa na NACTE DODOMA mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/BUG/RB/94859/2022.

## KIPOTEA KWA CHETI



MWAJUMA MUSSA IDDI anatangaza kupotelewa na cheti cha kozi ya UALIMU chenye registration namba ITC/2014/DECE/8894 kilichotolewa na chuo cha UALIMU-ILONGA mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa SAM/RB/149/2022**

---

**Magistrate Court (approved forms for the Primary Court)**

**GN.NO.943 (Contd.)** **FOMU MADAI-3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya Wilaya Kigoma**

**Kituo cha Ujiji Mkoa wa Kigoma**

**SHAURI LA MADAI NA 30……MWAKA…….2021**

**JINA LA MDAI. KAMANGA KASANGA WATENDELE**

**JINA LA MDAIWA. NAIMANA STUMAI RUZENDUKA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo).**

**Kwa …….NAIMANA STUMAI RUZENDUKA…………**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba (eleza habari za madai)………….anakudai kiasi cha fedha Tsh. 1487,000 kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe…29….Mwezi…03….Mwaka…2022…… saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe…..02…..Mwezi….03…Mwaka…..2022……………………………**

**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya ya Morogoro**

**Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 19…..2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ISSA KUDURA……WA Kihonda**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SELESTINI SANGAGA.**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 07/03/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA.170/17/ YA 2020**

**DHIDI YA**

**TITO PATRICK SANGA……………MLETA MAOMBI**

1. **ESMAIL YARU MOHAMED**
2. **ERIC AUCTION MART**
3. **ASIA DISMAS CHALE**
4. **FADHIL JUMA……………WAJIBU MAOMBI**

**KWA.FADHIL JUMA**
**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la maombi madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na mahakama hii hapa dar es salaam tarehe 14/03/2022 saa mbili na dakika arobaini na tano asubuhi (08.45).

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutaudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetembulika kisheria basi maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wako

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 02/03/2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**IKIKETI BUKOBA**
**MIS LAND CASE APPLICATION 34 OF 2021**
**Ikitokana na land Appeal No.28 of 20219 ya Mahakama kuu Bukoba**
**Shauri la awali land application no.45 of 2022**
**Katika Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya Bukoba**
**DEOGRATIAS KASSINDA……… MUOMBAJI**
**Dhidi ya**
**MAKIU KAJWANGYA…..MJIBU MAOMBI WA KWANZA**
**KANDIDA MTEFUNYA……… MJIBU MAOMBI WA PILI**
**KADINDA MTEFUNYA**
**KITONGOJI CHA BUGOMBE KATA KANYIGO - MISSENYI**

**YAH: TAARIFA YA SIKU YA KUSIKILIZWA**

Kwa kuwa mleta maombi DEOGRATIAS KASSINDA amewasilisha maombi yake dhidi yako, yaliyosajiliwa kama MISC LAND CASE APPLICATION 34 OF 2021. unapewa taarifa ya kwamba maombi hayo yamepangwa kusikilizwa tarehe 24/03/2022 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji Mwipopo.

Unatakiwa kuhudhuria wewe mwenyewe au kupitia kwa wakili wako. Unapewa taarifa zaidi kwamba kushindwa kuhudhuria kwako muda na tarehe iliyopangwa maombi hayo yatasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo siku ya jumatano tarehe 02/03/2022.

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**MOROGORO REGISTRY**
**LAND APPLICATION NO: 7 OF 2021**
**BETWEEN**

**ISMAIL MOHAMED AND TWO OTHERS**
**……….APPLLICANT**
**VERSUS**
**NURDIN KIGULUNUHA , ERASTO E. NGOWI , DISMAS MAGELE…..RESPONDENT**
**NOTICE OF MENTION**
**TO:**
**ERASTO E. NGOWI,DISMAS MAGELE**
**…………..RESPONDENT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on 24thday of March 2022 at 09:30 AM at the High Court of Tanzania at Morogoro.

Your required to appear in person or through your Advocate or Agents dully authorized to appear on your behalf.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the application for hearing in your absence.

**GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 21st day of February 2022.**

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**MOROGORO REGISTRY**
**LAND APPLICATION NO: 7 OF 2021**
**BETWEEN**

**ISMAIL MOHAMED AND TWO OTHERS**
**……….APPLLICANT**
**VERSUS**
**NURDIN KIGULUNUHA , ERASTO E. NGOWI , DISMAS MAGELE…..RESPONDENT**
**NOTICE OF MENTION**
**TO:**
**ERASTO E. NGOWI,DISMAS MAGELE**
**…………..RESPONDENT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on 24thday of March 2022 at 09:30 AM at the High Court of Tanzania at Morogoro.

Your required to appear in person or through your Advocate or Agents dully authorized to appear on your behalf.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the application for hearing in your absence.

**GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 21st day of February 2022.**

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 7….2022**
**MDAI: TINGETINGE SACCOS (KARUME MWINSHEHE)**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: MAGRETH MSOWOYA**
**Kwa: MAGRETH MSOWOYA**
**Ombi la mdai: TINGETINGE SACCOS (KARUME MWINSHEHE)**

Madai ya : Pesa Shillings 580,000/=

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 09 mwezi 03 mwaka 2022 saa2:30 asubuhi.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

**Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 07 mwezi 03 mwaka 2022.**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 15 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late EWARDA SEVELIN LIKELEKA**

By 1. KELVIN SEVELIN LIKELEKA
2. ………………………………..

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 9 day of March..2022

**Dated at Morogoro this 7th day of FEB..2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KIWANJA KINAUZWA

KIWANJA KIPO **KISUKURU SEGEREA JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA 24 MLABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA NA KINA HATI, BEI NI MILIONI 55. KWA MAWASILIANO **PIGA 0754 857523/0655 857523.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya NJOMBE**

**Kituo cha NJOMBE MJINI mkoa wa NJOMBE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 19/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA ROBERT KIPAKA MSENGA Marehemu Wa Mji Mwema**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa**

**NA: RENATUS ROBERT MSENGA mwombaji**

**TANGAZO KWA UMMA**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14//4/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo 16/02/2022

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 33 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late PETER BONA KASENYI**

**By 1. NEEMA ELIDORETH MBASHA**
**2. ……………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the16 day of 3 …2022

Dated at Morogoro this 4 day of 3 …2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MIRIAM JOEL LECHIPYA**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI (Nissan hommy) /bima ya ya gari na risiti ya veco inspection yenye namba za usajili **T 697 CUG (CHASSIS NO VRMGE24056120)** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0719599549**

**MOR /MOR/RB/78305/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RAMIA JUMA FUNDE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA MARK II yenye namba za usajili T 746 CUT,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa ARU/ARU/RB/96118/2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI.**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA.**
**Usimamizi wa mirathi Na 5 /2022.**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ISSA MOHAMED WA MGUMBU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANMSHA ISSA MOHAMED**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 mwezi 02 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe20 mwezi 1 mwaka 2022.

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI PICHA

# Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani



Waandishi wa habari wanawake wa Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, kwenye ofisi za TGL, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Katikati ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe. **PICHA: JOHN BADI**



Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara ya Taifa (NBC), Theobadi Sabi (kushoto), akiwahudumia chai wafanyakazi wanawake wa benki hiyo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Baadhi ya wafanyakazi wanawake na wanaume wa kampuni ya Barrick, wakiwa wameungana pamoja kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo katika mgodi wa dhahabu wa North Mara, wilayani Tarime jana, kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wanawake wa benki hiyo, wakionyesha ishara ya kuvunja upendeleo wa kijinsia ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu masuala mbalimbali ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kulia ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa kituo hicho, Silvan Sariko na Ofisa Programu, Wanawake na Watu wenye Ulemavu, Getrude Dyabene. **PICHA: SABATO KASIKA**

# AZAM YAZIACHIA SIMBA, YANGA UBINGWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Klabu ya Azam imetangaza rasmi kujiondoa kwenye mbio za kuusaka ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu, ikisema ni kutoutendea haki mpira wa miguu kama ikiendelea kusema ina nia hiyo kwa sasa, na badala yake imegeuzia macho yake kwenye michuano ya Kombe la FA, ili kupata nafasi ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', alisema baada ya kutopata ushindi kwenye mechi tatu mfululizo, hawawezi kujidanganya kuwa wanaendelea kuusaka ubingwa msimu huu.

"Hata kama tunaweza kushinda mechi zetu zote zilizobaki, lakini hatuwezi kuzifanya timu zilizoko juu yetu kupoteza mechi zao zilizobaki, kwa hiyo kilichobaki sisi tunageukia Kombe la FA ambalo liko ndani ya uwezo wetu, hili tunatakiwa kushinda tu basi, bila kusubiri nani apoteze. Kusema eti bado tuna ndoto za ubingwa ni kutoutendea haki mpira wa miguu," alisema Zaka Zakazi.

Azam Jumamosi iliyopita ilipoteza mechi kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ikiwa ni mechi ya tatu mfululizo kucheza si tu bila kupata ushindi, lakini kufunga bao.

Baada ya kuichapa Dodoma Jiji mabao 2-0 Februari 4, mwaka huu, Azam ilikumbana na kipigo cha 2-0 dhidi ya Biashara United ugenini, ikalazimishwa suluhu dhidi ya Coastal Union, kabla ya kupoteza kwa Polisi Tanzania.

"Tulipatwa na mshtuko baada ya kufungwa mabao 2-0 na Biashara United, inavyoonekana wachezaji wetu hawajarejea kwenye hali yao ya kawaida, ndiyo maana mechi hizi mbili pia tukafanya vizuri," alisema.

Azam inashika nafasi ya nne ikiwa na pointi 25 kwa mechi 17 ilizocheza hasa sasa.

## 'WANAWAKE DAY'...




Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Klabu ya Simba kwa kushirikiana na Mo Dewji Foundation imetembelea Gereza la Wanawake la Segerea na kutoa misaada ya huduma muhimu kwa wafungwa. Wapili kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, akikabidhi misaada hiyo ambayo ni pamoja na sabuni, sukari, taulo za kike na dawa za meno. Barbara aliambatana na Timu ya Wanawake ya Simba Queens pamoja na Kocha Mkuu, Sebastian Mkomwa. **PICHA: SIMBA**

# *Odhiambo achanga karata kuinusuru Prisons*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, amesema tayari ameweka mikakati ya kuhakikisha anaiondoa timu hiyo kwenye nafasi ya kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tanzania Prisons inaburuza mkia ikiwa na pointi 13, baada ya kushinda michezo mitatu sare nne na kupoteza 10 katika mechi 17 walizocheza za ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema mipango yake kwa sasa ni kuhakikisha wanashinda mechi zilizobakia za mzunguko wa pili ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuendelea kuwapo ligi msimu ujao.

Alisema kazi kubwa anayoifanya ni kuimarisha safu yake ya ulinzi ikiwamo kipa kutokana na kuruhusu mabao mengi, lakini akimulika suala la umakini kwa safu yake ya ushambuliaji kwani imekuwa ikipoteza nafasi nyingi za wazi.

"Tumekuwa katika hali mbaya tuko katika nafasi ya mwisho, tunataka kutoka hapa tulipo na kupanda juu ya msimamo, mipango yetu ni kuhakikisha tunashinda mechi hizi zilizobaki ili tuendelee kuwapo katika ligi kwa msimu ujao," alisema Odhiambo.

Alisema ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika michezo iliyobaki na kuendelea kuwapo kwenye Ligi Kuu msimu ujao. Timu mbili zitakazoburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo, zitashuka daraja moja kwa moja wakati zile zitakazoshika nafasi ya 13 na 14, zitacheza mechi ya mchujo 'play off' dhidi ya timu zitakazoshika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Championship kutoka Kundi A na B ili kuwania nafasi mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

## Kaseja atoa sababu kipigo KMC

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukubali kipigo cha mabao 3-2 nyumbani dhidi ya Coastal Union, kipa mkongwe nchini, Juma Kaseja ambaye alipewa jukumu la kulinda lango lao kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Azam Complex juzi, amesema "hatukuwa kwenye ubora wetu wa kawaida".

Kaseja ambaye alifungwa bao la penalti na Abdu Selemani 'Sopu', ikiwa ni nadra sana kwa kipa huyo kufungwa katika matuta, alisema kulikuwa na matatizo mengi kwenye mechi hiyo na makosa kadhaa, ndiyo yaliyosababisha kupoteza mechi hiyo.

"Tumefungwa kwa sababu hatukucheza vizuri, tumeruhusu mabao mengi rahisi, kusema kweli hatukuwa kwenye ubora wetu na haikuwa KMC ile ambayo ilicheza mechi mbili za nyuma. Kulikuwa na matizo mengi na makosa kadhaa, lakini niseme ndiyo mpira na huenda Mungu aliwapangia Coastal Union kushinda kwa sababu hawajashinda kwa muda mrefu," alisema Kaseja.

Kwa upande wa Sopu alisema ushindi walioupata utawafanya kuanza kujiamini na kuendeleza wimbi la ushindi baada ya kupita muda mrefu.

"Tumecheza mechi nyingi hatujashinda, hata mechi hii ilikuwa ni ngumu, lakini wachezaji tumejituma sana, na umeona hata bao la tatu limefungwa dakika za mwisho kabisa," alisema winga huyo. Coastal Union ilicheza mechi sita mfululizo bila kupata matokeo, huku ikiwa haijashinda tangu kuingia mwaka mpya wa 2022.

Mara ya mwisho iliifunga Mbeya City mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Desemba 24, mwaka jana, na kuanza kazi ya kusaka ushindi mwingine hadi ilipoupata kama huo juzi. Matokeo hayo yanaiweka KMC kwenye nafasi ya sita kwa pointi 22, na Coastal Union ikikaa nafasi ya 10 kwa kufikisha pointi 21.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KWENDA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo huenda akahamia Paris St-Germain, ambayo inapania kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 kuungana na mshindani wake, Lionel Messi mwenye miaka 34, ikiwa Manchester United itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. (***Football Transfers)***

### RASHFORD AWINDWA ARSENAL

ARSENAL, Newcastle na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia mshambuliaji wa England, Marcus Rashford huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, akiaminika kufikiria hatima yake Manchester United. (***90Min)***

### PSG NAO WATUA UNITED

KLAB ya Paris St-Germain pia itajaribu kumsaini Rashford ikiwa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, atajiunga na Real Madrid. PSG ilijaribu kumsajili Rashford msimu uliopita, lakini Manchester United hawakuwa tayari kumuuza. ***(Mail)***

### CITY, MADRID KWA HAALAND

MANCHESTER City na Real Madrid ni klabu mbili zinazoongoza katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland licha ya Bayern Munich na Barcelona kuonyesha nia ya kumtaka. Hatima ya Haaland mwenye umri wa miaka 21 raia wa Norway inatarajiwa kuamuliwa katika "wiki chache zijazo ". (***Athletic***)

### ARSENAL, PSG KWA PAQUETA

ARSENAL ipo tayari kushindana na Paris St-Germain katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 24 kutoka Lyon. ***(Calciomercato)***

### JOHNSON AITAKA CHELSEA

MMILIKI wa Klabu ya New York Jets, Robert Wood Johnson, anajiandaa kutoa ofa ya kuinunua Chelsea. Johnson anachukuliwa kuwa "mjuzi sana" wa klabu hiyo na aliwahi kuishi London kama balozi wa Marekani nchini Uingereza. (***ESPN***)

### HAZARD ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imeanzisha mazungumzo na Real Madrid kuhusu usajili wa mchezaji nyota wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31, ambaye anatarajiwa kuondoka mji huo mkuu wa Hispania msimu wa majira ya joto. ***(Defensa Central***)

### RANGNICK AKEJELIWA UNITED

BAADHI ya wachezaji wa Manchester United wameonyesha kukejeli uwezo wa kocha wa muda, Ralf Rangnick na kutoridhishwa na mbinu za raia huyo wa Ujerumani. ***(MEN***)

### MARTINELLI KUBAKI ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 20, amesema anataka kubaki Arsenal. (***Liverpool Echo***)

### NKUNKU AWANIWA CHELSEA

CHELSEA na Manchester City ni miongoni mwa klabu zinazomnyatia kiungo wa kati wa RB Leipzig, Christopher Nkunku. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, huenda akagharimu karibu pauni milioni 62. ***(Foot Mercato, via Express***)

### MATA KUONDOKA UNITED

JUAN Mata ataondoka Manchester United kama mchezaji huru msimu wa majira ya joto huku kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 33, akitakiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu Hispania, LaLiga. ***(Athletic***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE SHAKANI KUIVAA MADRID LEO

## Anasumbuliwa na mguu wa kushoto baada ya kupata maumivu kwenye mazoezi juzi...

**PARIS,** UFARANSA

MSHAMBULIAJI nyota wa Timu ya Paris St Germain, Kylian Mbappe, amepata majeraha ya mguu akiwa mazoezini na bado kuna wasiwasi ikiwa atakuwa sawa kuwavaa Real Madrid kwenye mzunguko wa pili wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya leo, Jumatano.

Mbappe ndiye mfungaji pekee wa bao la Paris St Germain kwenye mchezo wa kwanza na kufanya mechi kumalizika kwa ushindi wa 1-0 mwezi uliopita.

"Kylian Mbappe anasumbuliwa mguu wa kushoto baada ya kupata maumivu kwenye mazoezi jana (juzi)," taarifa ya PSG ilisema.

**"Alitibiwa mchana wa leo (jana), wataalamu wanaji hakikishia na watamfanyia tena vipimo baada ya saa 24."**

Mbappe aliukosa mchezo wa Jumamosi ambao PSG walipoteza dhidi ya Nice kwa bao 1-0 kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kutokana na adhabu.

PSG walikataa ofa mbalimbali kutoka kwa Real Madrid kwa ajili ya kumbakisha Mbappe mwenye umri wa miaka 23, ambaye mwisho wa msimu huu anaweza kuondoka kama mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,013

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 2.55
X | 3.53
2 | 2.60

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHRISTENSEN AKUBALI MIAKA 5 BARCELONA



**LONDON,** England

TAARIFA zinasema kuwa mlinzi wa Chelsea, Andreas Christensen, tayari amekubali kuungana na Barcelona.


Kwa mujibu wa mwandishi wa habari maarufu wa habari za michezo wa Italia, Fabrizio Romano na gazeti la Mundo Deportivo, nyota huyu tayari amekubali kuungana na Barcelona kwa dili la miaka mitano.

Mkataba wa Christensen na Chelsea unamalizika Juni 30, na kwa takriban wiki kadhaa Barcelona wamekuwa wakizungumza na wakala wa nyota huyo.

Ikiwa dili hili liko sawa, Christensen anatarajia kuwasili Camp Nou, baada ya Mkurugenzi wa Michezo, Mateu Alemany na Jordi Cruyff kusafiri kwenda London.

Christensen ana umri wa miaka 25 tu, lakini tayari ana uzoefu mkubwa na ni sehemu muhimu ya kikosi cha Chelsea kilichowachapa Manchester City na kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bayern Munich pia walitajwa kuiwania saini yake, lakini nyota huyo anatajwa kuwa na mahaba ya kuichezea Barcelona chini ya Xavi Hernandez.



## 'Kama si Liver, City mabingwa Feb'

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jürgen Klopp amedai kuwa timu ya Manchester City wangetawazwa mabingwa wa Ligi Kuu England Februari kama Liverpool isingekuwapo.

Man City na Liverpool ndani ya miaka minne wamekuwa wakibadilishana mataji kati yao.

Man City ametwaa taji hilo mara tatu, Liverpool akiwa amechukua mara moja, huku wakiwa wanafukuzana kwenye mbio za ubingwa mwaka huu, ambapo Pep Guardiola na timu yake wako kileleni kwa tofauti ya pointi tatu.

Klopp wakati akizungumza na waandishi wa habari alinukuliwa akisema, "ni ligi ngumu duniani, hakuna shaka kwenye hilo, lakini ni changamoto, na hakika tunafurahia, kama tusingekuwapo hapa mwaka huu au miaka miwli iliyopita au mitatu basi Manchester City angekuwa bingwa Februari."

"Sababu tupo hapa, ni ngumu. Kama Manchester City wasingekuwapo hapa nadhani tungekuwa na nafasi ya kuwa mabingwa."

Awali Guardiola aliwahi kuiita timu ya Liverpool kuwa ni washindani imara ambao hajawahi kukutana nayo tangu aanze kazi yake ya kuwa kocha, na Klopp naye amesema sawa sawa kuhusu City na kutoa sifa zake kwa kocha huyo.

## HABARI MICHEZO


# 3,643,920 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/03/22 | 18:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 02. 12/03/22 | 18:00 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 03. 12/03/22 | 18:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 04. 12/03/22 | 19:00 | Montpellier vs Nice | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 05. 12/03/22 | 23:00 | Troyes vs Nantes | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 06. 12/03/22 | 23:00 | Getafe vs Valencia | 2.46 | 3.06 | 3.06 |
| 07. 12/03/22 | 23:30 | Belenenses vs Boavista | 2.71 | 3.25 | 2.51 |
| 08. 13/03/22 | 14:15 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.80 | 3.35 | 2.48 |
| 09. 13/03/22 | 15:00 | Luton Town vs QPR | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 10. 13/03/22 | 15:30 | Hannover vs Nurnberg | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 11. 13/03/22 | 17:00 | Angers vs Reims | 2.27 | 3.13 | 3.28 |
| 12. 13/03/22 | 17:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.37 | 3.32 | 2.92 |
| 13. 13/03/22 | 17:00 | Everton vs Wolverhampton | 2.29 | 3.26 | 3.16 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 09/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1524 | Oita Trinita vs Mito Hollyhock | 2.21 | 2.98 | 3.22 |
| 14:00 | 5923 | Buriram Utd vs Chonburi | 1.47 | 4.06 | 5.80 |
| 15:00 | 2993 | Irodotos vs Egaleo Athens | 2.74 | 2.79 | 2.65 |
| 15:00 | 5065 | ASK Bravo vs Tabor Sezana | 1.97 | 3.13 | 3.67 |
| 15:30 | 3280 | AL Ain vs AL Draih | 2.31 | 2.88 | 3.13 |
| 15:30 | 4806 | Port FC vs Chiangrai Utd | 2.19 | 3.13 | 3.09 |
| 15:40 | 4297 | AL Adalh vs AL Nahdha | 1.57 | 3.46 | 5.77 |
| 16:00 | 1460 | Renova vs Shkupi Skopje | 3.95 | 3.37 | 1.82 |
| 16:00 | 2312 | Ghazl EL Mahallah vs Coca Cola | 3.69 | 2.85 | 2.20 |
| 16:00 | 2325 | Apollon 1926 vs AO Trikala | 1.76 | 3.28 | 4.44 |
| 16:00 | 2594 | Akademija Pandev vs FK Borec | 1.39 | 4.15 | 7.15 |
| 16:00 | 2866 | AEK Athens B vs Diagoras FC | 1.43 | 3.76 | 7.52 |
| 16:00 | 2976 | Rhodos FC vs O F Ierapetras | 2.70 | 2.84 | 2.65 |
| 16:00 | 3272 | PO Triglias vs Apollon Larisas | 1.55 | 3.38 | 6.37 |
| 16:00 | 3462 | Episkopi FC vs APS Zakynthos | 1.57 | 3.43 | 5.79 |
| 16:00 | 3551 | Levadiakos vs Kallithea FC | 1.51 | 3.55 | 6.33 |
| 16:00 | 4066 | III Ker Tue Upe vs Soroksar | 2.59 | 3.27 | 2.45 |
| 16:00 | 4171 | Bregalnica Stip vs FK Pelister Bitola | 1.27 | 4.82 | 9.44 |
| 16:00 | 4251 | Pierikos Katerini vs Olympiakos Volos | 2.33 | 3.18 | 2.80 |
| 16:00 | 4361 | SKODA Xanthi vs Niki Volou | 1.46 | 3.73 | 6.78 |
| 16:00 | 4631 | Rabotnicki Sk vs Shkendija | 5.99 | 3.72 | 1.51 |
| 16:00 | 5114 | Kalamata FC vs AE Asteras Vlachioti | 1.21 | 4.85 | 14.55 |
| 16:00 | 5539 | Kifisias vs Kissamikos | 2.65 | 2.94 | 2.61 |
| 16:00 | 5833 | FC Struga Trim Lum vs Makedonija GjP | 1.90 | 3.08 | 4.04 |
| 16:30 | 4842 | RC Relizane vs JS Saoura | 5.97 | 3.18 | 1.62 |
| 16:30 | 5807 | FC Veria vs AE Larissa | 2.16 | 3.09 | 3.19 |
| 17:00 | 2170 | MSK Zilina vs Komarno | 1.22 | 6.17 | 8.29 |
| 17:00 | 4126 | NK Celje vs Domzale | 2.33 | 3.14 | 2.85 |
| 18:00 | 4441 | Ethnikos Achnas vs EN Paralimni | 1.84 | 2.93 | 4.61 |
| 18:30 | 2572 | Slovan Liberec vs Pardubice | 1.58 | 4.11 | 5.41 |
| 18:30 | 3949 | Talaea El Gaish vs Al Masry Club | 2.91 | 2.62 | 2.86 |
| 19:00 | 2158 | Iskra vs Petrovac | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 19:05 | 3190 | Jeddah Club vs Najran SC | 2.31 | 2.79 | 3.23 |
| 19:30 | 2894 | NK Radomlje vs Luka Koper | 2.74 | 3.61 | 2.18 |
| 20:00 | 1208 | LKS Lodz Pss vs Puszcza Niepolomice | 1.74 | 3.37 | 4.34 |
| 20:00 | 2086 | Pecs MFC vs Vasas SC | 3.55 | 3.60 | 2.01 |
| 20:00 | 3204 | Szeged vs Budaors | 1.52 | 4.20 | 6.00 |
| 20:00 | 4338 | Apoel Nicosia vs Anorthosis Famagusta | 2.06 | 3.09 | 3.43 |
| 20:00 | 4654 | HNK Rijeka vs NK Osijek | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 20:00 | 4751 | SV Lippstadt 08 vs Wegberg-Beeck | 1.58 | 3.82 | 4.83 |
| 20:45 | 4124 | Porto vs Lyon | 2.04 | 3.51 | 3.51 |
| 20:45 | 4272 | Betis vs Eintracht Frankfurt | 1.86 | 3.66 | 4.01 |
| 21:00 | 2945 | Berliner Dynamo vs Babelsberg | 1.27 | 5.42 | 7.93 |
| 21:00 | 4035 | Flora Tallinn vs Levadia Tallinn | 2.13 | 3.57 | 2.85 |
| 21:00 | 4807 | Wuppertal vs SV 19 Straelen | 1.36 | 4.42 | 7.11 |
| 22:45 | 2238 | Cray Wanderers vs Haringey Borough | 2.27 | 3.82 | 2.51 |
| 22:45 | 3743 | Hartlepool vs Rotherham | 5.20 | 4.05 | 1.51 |
| 22:45 | 3892 | Dundee FC vs St Mirren | 2.91 | 3.06 | 2.47 |
| 23:00 | 2433 | Manchester City vs Sporting Lisbon | 1.18 | 6.76 | 15.58 |
| 23:00 | 4638 | Real Madrid vs Paris St Germain | 2.55 | 3.53 | 2.60 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# *SportPesa, Airtel Money, M-Pesa wazindua 'Bet Bonanza'*



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, akizungumza na waandishi wa habari kwenye uzinduzi wa Promosheni ya Bet Bonanza iliyofanyika Masaki, Dar es Salaam jana, Wapili kushoto ni Meneja Mauzo Kitengo cha M-Pesa, Kelvin Nyanda, akifuatiwa na Meneja Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya na kulia ni Aggrey Charles, Meneja Mauzo Biashara, Airtel Money. **PICHA: SPORTPESA**

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo na burudani ya SportPesa, imezindua rasmi kampeni maalum kwa ajili ya kuwazawadia wateja wake.

**Katika promosheni hiyo ambayo ilizinduliwa rasmi jana Masaki, Dar es Salaam ikihusisha kampuni za mitandao ya simu, Vodacom na Airtel ikiwa na lengo la kuwazawadia wateja hasa katika kipindi hiki ambapo mechi mbalimbali zinaendelea.**

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Sportpesa, Tarimba Abbas, alisema katika kipindi hiki tumeona tuwazawadie wateja wetu wote kwa kuzindua promosheni inayoenda kwa jina la "Bet Bonanza".

"Promosheni hii inaanza rasmi leo (jana) na itadumu kwa muda wa siku 35. Kutakuwa na washindi wa kila siku ambao watajishindia kiasi cha shilingi 20,000 kila mmoja, kila siku, na washindi wa shilingi milioni moja moja kila wiki na mwisho wa promosheni tutatoa 15,888,000/- kwa mshindi mwenye bahati.

"Droo zitachezwa kila siku na washindi watatangazwa kupitia kurasa za mitandao ya kijamii zetu na za washirika wetu Vodacom, na Airtel, pamoja na kurasa za timu tunazozidhamini Simba, Yanga na Namungo," alisema Tarimba na kuongeza:

"Ili kushiriki kwenye promosheni hii, ni lazima kuweka pesa kwenye akaunti yako ya SportPesa na kuanza kucheza ili kuingia kwenye droo ili na kupata nafasi ya kuibuka mshindi, kwa wateja wapya watatakiwa kujisajili kwanza kisha kufuata mtiririko huo huo.

"Napenda kuwakaribisha watumiaji wa mitandao yote kushiriki kwenye promosheni hii hata wale ambao hawajajisajili na SportPesa ili waweze kushinda zawadi za kila siku, kila wiki na zawadi kubwa kabisa ya zaidi ya shilingi milioni 15."

Kwa upande wa Meneja Mauzo wa M-Pesa, kutoka Kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, Kelvin Nyanda, alisema, wameamua kushirikiana na Sportpesa kwa sababu kuna ligi mbalimbali zinazoendelea kama Champions League (Ligi ya Mabingwa), NBC Premier League, English Premier League, Legue 1 na nyinginezo ambazo zitawapa fursa wateja wao kwa siku 35 kujinyakulia kiasi cha Sh. 20,000 kila siku, milioni moja moja kwa wiki na zawadi kubwa ya zaidi ya Sh. milioni 15, mwisho wa kampeni."

"Kushiriki ni rahisi sana, kila mteja wa M-Pesa ana nafasi ya kushinda katika kipindi hiki kwa kuingia kwenye 'menyu' ya malipo ya M-Pesa kisha chagua lipa bili, halafu michezo, kisha SportPesa, halafu fuata maelezo.

"Ukimaliza utapata majibu papo hapo kuwa umeingia kwenye droo ya siku/wiki/mwezi, na washindi watapigiwa simu kujulishwa kuwa wameshinda na majina yatatangazwa kwenye kurasa za mitandao ya kijamii (Social media pages) za SportPesa.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wateja wetu kushiriki mara nyingi wawezavyo, maana ushindi upo kwa ajili yao," alisema.

Akizungumza kutoka Airtel Meneja Mauzo, Biashara, Aggrey Charles alisema: "Katika msimu huu kuna mechi mbalimbali zinaendelea tumeona ni vizuri kushirikiana na washirika wetu SportPesa ili wateja wetu wa Airtel waweze kubashiri kwa urahisi na kupata nafasi ya kujishindia mamilioni ya pesa.

"Kushiriki ni rahisi, mteja wa Airtel anapaswa kujisajili na Sportpesa na kuweka pesa kwenye akauti yake ya SportPesa kupitia huduma ya Airtel Money kubashiri mechi anayoipenda na kupata nafasi ya kuingia kwenye droo ili kujishindia zawadi za kila siku, wiki na hatimaye zawadi ya mwisho wa promosheni ambayo ni shilingi 15,888,000.

"Kumbuka mteja wa Airtel kupitia huduma ya Airtel Money anaweza kuweka pesa kwenye akaunti ya SportPesa kwa kupiga *150*60# au kupitia Airtel Money App au kupitia www.sportpesa.co.tz."

Michezo
Jumatano Machi 9, 2022
Nipashe



Mbappe shakani kuivaa Madrid leo
UKURASA 21

# Pablo apata jeuri silaha za kuimaliza RS Berkane

## ●●● Atamba morali kuwa juu na upana wa kikosi baada ya...

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata juzi kwenye Ligi Kuu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Dodoma Jiji FC, ambao umekuja siku tatu baada ya kuichapa Biashara United 3-0 uwanjani hapo, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameunganisha na sababu nyingine akisema ni ishara nzuri kuelekea mechi yao ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane ya Morocco.

**Simba itaikaribisha RS Berkane Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, huo ukiwa ni mchezo wa marudiano wa Kundi D la michuano hiyo, baada ya Wamorocco hao mchezo wa awali kushinda 2-0 wakiwa nyumbani.**

Lakini baada ya kushinda mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji juzi, Pablo alisema ushindi huo utaongeza morali na hali ya kujiamini kwa wachezaji wake kuelekea maandalizi ya mchezo wao dhidi ya RS Berkane.

Pablo alisema walicheza vizuri na kutengeneza nafasi nyingi huku wakitawala sehemu kubwa ya mchezo, lakini kipindi cha kwanza hawakuweza kutumia vema nafasi walizotengeneza.

Alisema pia jambo zuri kwao kuelekea mechi hiyo dhidi ya Berkane, ni upana wa kikosi baada ya wachezaji waliokuwa majeruhi wa muda mrefu kurejea na juzi kupata nafasi dakika chache ili kuwarejesha katika hali za kawaida na kuwa tayari kwa michezo ijayo ikiwamo huo wa kimataifa.

"Ushindi huu umeongeza morali kuelekea mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya RS Berkane, tunaenda kufanya maandalizi mazuri kabla ya mchezo huu ambao ni muhimu kwetu kupata matokeo mazuri nyumbani," alisema Pablo.

Kwa upande wa Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wanamshukuru Mungu kupata ushindi huo na kwamba wapinzani wao, Dodoma jiji FC walicheza mpira mzuri.

Alisema mpira waliocheza Dodoma Jiji uliwapa upinzani mkubwa kuelekea mchezo dhidi ya RS Berkane.

"Tuwapongeze wapinzani wetu kwa kucheza mpira mzuri na kuleta upinzani mkubwa kwetu kwa sababu hii ni mechi halisi tuliyopata ya ushindani kuelekea mchezo wetu wa kimataifa," alisema Ahmed.

Kuhusu suala la penalti Ahmed alisema bado shida hiyo ipo na kocha Pablo anaifanyia kazi taratibu, baada ya mechi dhidi ya Biashara United, Meddie Kagere kukosa kabla ya juzi dhidi ya Dodoma Jiji, Clautos Chama kufunga.

"Hii shida haitaisha kwa haraka, mechi iliyopita tulikosa kupitia kwa Kagere, lakini leo (juzi) tumepata kupitia Chama, tatizo hili haliwezi kumalizwa kwa haraka, ni taratibu na baadaye tutakuwa sawa," alisema Ahmed na aliongeza:

"Malengo yetu ya kurejea katika nafasi ya kwanza bado yako pale pale, huu ni ushindi wetu wa pili na mabao matano kwenye mzunguko wa pili na jumla tumecheze mechi 17 kuna mechi nyingi bado ziko mbele yetu hivyo tunatarajia kufanya vizuri katika michezo hiyo na kupata pointi," alisema Ahmed.

Alisema kurejea uwanjani kwa nyota wao wawili, Kibu Denis na Taddeo Lwanga kwa kucheza kwa kiwango bora kunaonyesha matumaini makubwa ya kurudi katika ubora wao na kusaidia timu hiyo.

"Wale tulishacheza nao wanashukuru, kazi kubwa inakuja kwa ambao bado hatujacheza hasa baada ya kurejea uwanjani na kupona wachezaji hao nina imani tutaleta maafa huko mbele," alisema Meneja huyo wa Simba.

Alisema Simba haitegemei mshambuliaji mmoja kama akikosekana huyo basi ni mtihani, kwani kwa upande wao kuna zaidi ya mmoja katika safu ya ushambuliaji na wote wanapata nafasi na wanauwezo wa kufunga.

"Ukiangalia washambuliaji wetu wote wako vizuri na wakipata nafasi wanafunga, kuhusu John Bocco hiki kipindi cha mpito kinapita atarejea, Simba hatumtegemei mtu mmoja kama ilivyo kwa wengine," alisema Ahmed.

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Simba, Clautos Chama (juu) na Pascol Wawa wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju. Miamba hao watashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili kuikaribisha RS Berkane ya Morocco kwenye mechi ya marudiano ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga wafunguka majeraha ya Mayele

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa straika wake, Fiston Mayele ambaye aliumia kwenye mechi dhidi ya Geita Gold iliyochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na kufunga bao pekee wakati wakishinda 1-0, anaendelea vema na kama hali ikiendelea vizuri huenda akawapo tena kwenye mechi ijayo dhidi ya KMC Machi 16, mwaka huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, jana alisema mchezaji huyo ambaye alipata majeraha kwenye mechi hiyo anaendelea vizuri, lakini madaktari ndiyo watakaotoa taarifa rasmi nao watazifikisha kwenye vyombo vya habari.

"Majeruhi wetu wanaendelea vizuri, Mayele anaendelea vema, alipata mushkeli kwenye mechi yetu dhidi ya Geita Gold, kwa mwonekana hana tatizo kubwa, lakini madaktari watamwangalia zaidi kwa sababu wao ndiyo wanaopima na kuona ukubwa wa jeraha na kutoa mapendekezo nini cha kufanya," alisema Bumbuli.

Kuumia kwa Mayele kulizua hofu kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa Yanga, huku wakitaniwa na watani zao wa jadi kuwa anaweza kukaa nje kwa muda mrefu, kitu ambacho kitaiathiri timu hiyo, kwani ameonekana kuwa ndiye tegemeo zaidi kwenye ufungaji.

Bumbuli alisema kuwa Yanga itaanza mazoezi leo baada ya kupewa mapumziko mafupi waliporejea kutoka Mwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002